# TASWIRA YA GEREZA INAVYOENDELEZA MAUDHUI KATIKA RIWAYA YA *HAINI* YA ADAM SHAFI.

NA

GERALD OKIOMA MOGERE

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

JUNI, 2007

University of NAIROBI Library
0370741 1

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya Shahada katika chuo kikuu kingine chochote.

...............................................................................................

Gerald Okioma Mogere

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na chuo kikuu.

...............................................................................................

Dkt. Tom Olali

(Msimamizi)

...............................................................................................

Mwalimu Swaleh Amir

(Msimamizi)

## TABARUKU

Kwa binti zangu: Cynthia na Syntyche. Mungu awabariki na awajalie wema na maisha mema.

## SHUKRANI

Namshukuru mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na uwezo wa kukamilisha tasnifu hii. Pia nawashukuru wote walionisaidia kwa hali na mali kukamilisha kazi hii. Nawashukuru wote hata kama sitawataja katika tasnifu hii.

Shukrani za kwanza nazitoa kwa wasimamizi wangu katika kazi hii: Dkt Tom Olali na Mwalimu Swaleh Amiri. Ahsante kwa kunipa mwongozo na mwelekeo katika utafiti huu. Nawashukuru pia, mwenyekiti wa idara Dkt Mwenda Mbatiah pamoja na Mratibu wa utafiti Idarani, Dkt. Jayne Mutiga. Nawashukuru wahadhiri wengine katika idara ambao mihadhara na mafunzo yao yamechangia pakubwa katika kutimiza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili. Hawa ni pamoja na: Prof. H.Abdulazizi, Prof. L. Omondi, Dkt. K. Mutiso, Dkt. J. Habwe, Dkt. K. Wamitila, Dkt. Z. Omboga na Mwalimu G. Mungania. Aidha, nawashukuru wahadhiri wote katika idara ya Isimu na Lugha.

Nawashukuru wenzangu ambao tuliabiri katika jahazi moja la usomi: Henry Njoroge, John Mutua, Samson Ongarora, Enoch Matundura, Evans Ogoro na Gabriel Kioni. Aidha sitawasahau wenzangu wa Isimu, Were, Florence, Nzioka, Obinchu, Nderitu, Aura, Jebet na Jackie.

Shukrani za dhati zimwendee mamangu, Bi. Coroneria. Ahsante mama kwa malezi mema na kujitolea kunielimisha. Vilevile nawashukuru ndugu zangu ambao wamejitolea kwa hali na mali kutimiza mahitaji ya masomo yangu. Hawa ni: Joseph, Simeon, Charles, Ann, Wilfred na Chrisantus, pamoja na familia zao.

Kwa njia ya kipekee namshukuru mke wangu mpendwa, Dinah, pamoja na binti zangu Cynthia na Syntyche. Ahsanteni kwa kuvumilia nilipokuwa mbali nanyi kwa minajili ya kusoma.

Hatimaye nawashukuru enyi binamu zangu, Peter na Ombongi kwa kunifaa kwa hali na mali siku nilipokuwa Nairobi. Nawe Rachel, sitakusahau kwa kunifanyia kazi bora ya kuipiga chapa tasinifu hii.

Mungu awabariki nyote.

Juni, 2007

Mogere O. Gerald

## IKISIRI

Tasnifu hii imechunguza namna taswira ya gereza inavyotumiwa kuendeleza maudhui katika *Haini* riwaya ya Adam Shafi. Tasnifu hii ina sura tano.

Katika sura ya kwanza, tumeshughulikia tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua somo, msingi wa nadharia, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu somo na vilevile njia tulizozitumia katika utafiti huu.

Katika sura ya pili, tumefafanua dhana muhimu tunazitumia katika utafiti huu. Tumezifafanua dhana za taswira, maudhui, gereza na jamii ya kigereza. Ufafanuzi wa dhana hizi umekuwa muhimu kwa kuwa umeweka misingi ya kukusanya na kuchanganua data ya utafiti wetu.

Sura ya tatu imeangazia namna sifa za jamii ya kigereza zinavyojitokeza katika *Haini.* Kwa hivyo, katika sura hii tumefafanua namna maudhui ya jamii ya kigereza yanavyosawiriwa na kuendelezwa riwayani.

Baada ya kuonyesha namna sifa za jamii ya kigereza zinavyojitokeza riwayani, sura ya nne imeonyesha athari za jamii ya Kigereza kwa mujibu wa riwaya ya *Haini.*

Sura ya tano ni hitimisho la utafiti wetu. Katika sura hii, pia tumetoa mapendekezo ya utafiti zaidi kuhusu riwaya hii ya *Haini.*

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| k.h.j | - Kama hapo juu |
| uk | - Ukurasa |

# YALIYOMO

**UNGAMO** ........ i

**TABARUKU** ........ ii

**SHUKRANI** ........ iii

**IKISIRI** ........ v

**VIFUPISHO** ........ vi

**YALIYOMO** ........ vii

**SURA YA KWANZA** ........ 1

1.0Utangulizi ........ 1

1.1 Tatizo la Utafiti ........ 3

1.2 Madhumuni ya Utafiti ........ 4

1.3 Nadharia Tete ........ 4

1.4 Sababu za Kuchagua Somo ........ 5

1.5 Msingi wa Nadharia ........ 5

1.6 Upeo na Mipaka ........ 9

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu somo ........ 10

1.8 Njia za Utafiti ........ 13

Tanbihi........ 14

**SURA YA PILI** ........ 15

**MISINGI YA UHAKIKI** ........ 15

2.0 Utangulizi ........ 15

2.1 Dhana ya Taswira ........ 15

2.2 Maudhui ........ 18

2.3 Gereza na Jamii ya Kigereza. ........ 19

2.4 *Haini* :Mazingira ya Kisiasa, Kijamii na Kiuchumi ........ 25

2.5 Muhtasari wa *Haini* ........ 29

2.6 Hitimisho ........ 31

Tanbihi ........ 32

**SURA YA TATU ........ 33**

**MAUDHUI YA JAMII YA KIGEREZA KATIKA *HAINI*. ........ 33**

3.0 Utangulizi ........ 33

3.1 Adhabu ........ 35

3.1.1Gereza ........ 35

3.1.2Udhalimu na Ukatili ........ 39

3.1.2.1 Mazingira Dhalilishi ........ 41

3.1.2.2 Uhaba Wa Chakula ........ 44

3.1.2.3 Kunyimwa Huduma za Matibabu ........ 45

3.1.2.4 Kupigwa Kinyama ........ 46

3.1.2.5 Mateso ya Kisaikolojia ........ 49

3.2 Adhabu za Kigereza Katika Jamii Pana. ........ 50

3.3 Nguvu na Matumizi Mabaya ya Mamlaka ........ 52

3.4 Uchungulizi ........ 56

3.5Hitimisho ........ 58

**SURA YA NNE** ........ 59

**ATHARI ZA JAMII YA KIGEREZA KATIKA *HAINI*** ........ 59

4.0Utangulizi ........ 59

4.1Usaliti na Ubinafsi ........ 60

4.2Hofu ........ 64

4.3Ukosefu wa Haki ........ 68

4.4.Unafiki ........ 70

4.5Jitihada za Ukombozi ........ 72

4.6Hitimisho ........ 73

**SURA YA TANO** ........ 76

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** ........ 76

5.0Hitimisho ........ 76

5.1Mapendekezo ........ 79

Marejeleo ........ 80

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Tasnifu hii inashughulikia namna taswira ya gereza inavyotumiwa kuendeleza maudhui katika *Haini* riwaya ya Adam Shafi. Katika utafiti huu, tunachunguza maudhui ya jamii ya kigereza na kubainisha namna yanavyosawiriwa na kuendelezwa katika riwaya hii. Tumefafanua maana ya dhana ya taswira kama tunavyoitumia katika utafiti wetu. Tumefafanua maana ya jamii ya kigereza na sifa kuu za jamii ya kigereza kama zilivyofafanuliwa na Michel Foucault, ambaye ndiye mwasisi wa nadharia ya Ki-Foucault inayoongoza utafiti huu. Aidha tumeonyesha namna sifa hizi zinavyojitokeza katika *Haini.*

Katika *Haini*, Kigogo ambaye ni kiongozi wa taifa ameuwawa kwa kupigwa risasi na Hamduni. Watu wengi wanasakwa, kukamatwa na kuwekwa gerezani kwa Shutuma za mauaji. Hamza, kijana mwandishi wa habari ni mmoja wa watu wanaokamatwa na kutiwa gerezani. Sehemu kubwa ya hadithi inasimulia matukio na wahusika waliomo katika mazingira ya kigereza. Ni muhimu kutaja hapa kuwa, taswira kuu katika riwaya ya *Haini* ni taswira ya gerezani na jamii inayozungumziwa ni jamii ya kigereza.

Jamii ya Kigereza ni jamii ambayo inalandana na gereza. Utafiti huu unakusudia kuchunguza *Haini* kwa kuwa ni kazi ambayo imejengwa katika mazingira yanayoakisi gereza, kwa hivyo, itatoa mwanga mwafaka wa suala tunalolenga kulihakiki. Fasihi ya aina hii inaitwa fasihi ya kifungoni. Kwa Mujibu wa Mbatiah (2001:16), fasihi ya kifungoni, ni fasihi inayotungwa na mtunzi ambaye yumo kifungoni au aliyefunguliwa lakini anatunga

kuzungumzia tajriba zake akiwa gerezani. Fasihi ya aina hii aghalabu huficha mateso ya mfungwa, hubainisha ukosefu wa ubinadamu na utu na pia hutetea msimamo, matendo au mawazo yaliyompelekea kufungwa. Mifano ya aina hii ya fasihi katika kiswahili ni diwani ya Abdalla: *Sauti ya Dhiki* (1973); diwani ya Mazrui: *Chembe cha Moyo* (1988). Hivi karibuni kuna riwaya ya Adam Shafi: *Haini (2003).* Katika maandishi ya Kiingereza kuna mifano ya kazi za; Thiong'o: *Detained (1981);* Kihoro: *Never Say Die: The Chronicle of a Political Prisoner (1998);* Mandela: *My Struggle my Life (1990);* Sithole: *Letters From Salibury Prison (1976);* Kinyatti: *Kenya: A Prison Notebook (1996).* Hii ni mifano ya waandishi wa kiafrika. Katika fasihi ya magharibi[1], kuna maandishi mengi ya utanzu huu wa fasihi, mfano mzuri ni mkusanyiko wa maandishi ya gerezani wa Abramowitz (1943) *The Great Prisioners: The First Anthology of Literature Written in Prison.* Katika kazi hii Abromowitz amekusanya na kuchapisha maandishi mengi yaliyoandikwa gerezani. Miongoni mwa maandishi haya, ni maandishi ya mwanafalsafa maarufu aitwaye Socrates, maandishi ya Mtume Paulo na mengine mengi ambayo ameyakusanya kutoka sehemu mbalimbali za ulimwenguni na yaliyoandikwa katika nyakati tofauti tofauti. Kuna maandishi mengine mengi ya utanzu huu yaliyoaandikwa miaka ya hivi karibuni. Tumetoa mifano hii kuonyesha namna utanzu huu ulivyompana; kimaeneo na kiwakati. Kwa hivyo kuonyesha umuhimu wake katika fasihi, jambo linalotia msukumo wa kutahakiki kazi za aina hii katika fasihi ya Kiswahili.

Fasihi ya kifungoni hudhihirisha maudhui ya kipekee ambayo yamejengwa katika mazingira ya kigereza. Utafiti huu unaonyesha namna maudhui ya jamii ya kigereza yanavyosawiriwa katika *Haini.* Tunashughulikia maudhui haya kwa mtazamo wa taswira

ya gereza kwa kuwa huu ndio mwelekeo unaochukuana na nadharia inayoongoza utafiti wetu. Ni muhimu kudokeza kuwa kwa mujibu wa nadharia ya Ki-Foucault, gereza ni sitiari ya jamii zetu na kwa kutumia taswira hii Foucault anadokeza mfanano uliopo kati ya gereza na maisha yaliyo nje ya gereza.

Adam Shafi ni mmojawapo wa waandishi waliotoa mchango wa kutajika katika uandishi wa riwaya ya Kiswahili. Mulokozi (1997: 107) ana maoni sawa na haya anaposema kwamba, wanariwaya marehemu M.S. Abdulla, M.S. Mohamed na Adam Shafi wamekweza bunilizi ya Kiswahili hadi ngazi nyingine kimaudhui na kimtindo. Miongoni mwa kazi za kifasihi za Adam Shafi ni pamoja na *Kasri ya Mwinyi Fuad ( 1978), Kuli (1979), Vuta N' kuvute (1999)* na riwaya yake ya hivi karibuni, *Haini* (2003) ambayo tunaishughulikia katika utafiti wetu.

## 1.1 Tatizo la Utafiti

Katika tasnifu hii tunajishughulisha na namna taswira ya gereza inavyotumiwa kuendeleza maudhui katika *Haini.* Tunachunguza namna maudhui ya jamii ya kigereza yanavyosawiriwa na kuendelezwa katika riwaya hii. Riwaya ya *Haini* imejengwa katika mazingira yanayoakisi gereza. Taswira ya gereza ndiyo taswira kuu katika riwaya hii. Somo hili limeteuliwa ili kuchunguza namna taswira hii inavyoendeleza maudhui ya jamii ya kigereza katika *Haini.*

Somo hili limeteuliwa katika misingi kwamba, nathari za fasihi ya kifungoni kama *Haini* katika fasihi ya Kiswahili, hazijahakikiwa katika misingi ya nadharia ya Ki-Foucault.

Utafiti huu unatarajia kulichangia pengo hili na vilevile kutoa mchango katika kuendeleza uhakiki wa fasihi ya Kiswahili. Aidha, uhakiki wa kazi yoyote ya fasihi ni muhimu kwa kuwa ndio hukamilisha lengo la mwandishi. Kazi yoyote haikukamilika hadi pale itakaposomwa na kutolewa kauli[2]. Utafiti huu ni mchango katika kutoa kauli hiyo kuhusu riwaya ya *Haini*.

## 1.2 Madhumuni ya Utafiti

Lengo kuu katika utafiti wetu ni kuchunguza jinsi taswira ya gereza ilivyotumiwa kuendeleza maudhui katika *Haini*. Kwa kufanya hivyo tunadhamiria kutambua sifa za jamii ya Kigereza na kubainisha jinsi zinavyodhihirika katika kazi tunayoihakiki.

Fasihi huchota malighafi yake katika jamii inamokulia. Matukio na asasi mbalimbali katika jamii hutoa mchango mkubwa katika kukuza fasihi ya jamii hiyo. Gereza ni moja ya asasi katika jamii ambazo zimetoa mchango katika kuendeleza fasihi kimaudhui. Katika msingi huu, tumedhamiria kuchunguza mawazo ya Shafi kuhusu nafasi, jukumu na athari za mfumo wa Kigereza katika jamii, kwa kurejelea *Haini*.

Aidha, tumenuia kuifafanua na kuifasiri kazi tunayoihakiki kwa kina ili kuwanufaisha wasomaji wake na vilevile kuinufaisha fasihi ya Kiswahili kwa jumla.

## 1.3 Nadharia Tete

Utafiti huu unaongozwa na nadharia tete kwamba:

a) Jamii anayoisawiri mwandishi katika kazi yake ni jamii yenye mwelekeo wa kigereza.

b) Maudhui ya jamii ya kigereza yamesawiriwa na kuendelezwa katika viwango mbalimbali ambavyo vinaiathiri jamii kwa namna mbalimbali.

c) Uhakiki wa Ki-Foucault unatoa mwelekeo mwafaka wa kuihakiki *Haini* kwa upande wa maudhui.

## 1.4 Sababu za Kuchagua Somo

Tumechagua somo hili kwa sababu ya uzito wake katika fasihi. Maudhui ni kipengele muhimu katika kazi ya fasihi, yanapofafanuliwa na kueleweka na wasomaji, lengo la mwandishi hukamilika.

Mpaka sasa utafiti uliofanywa katika fasihi ya Kiswahili haujamlika suala la jamii ya kigereza. Tumeonelea kwamba, pana haja ya utafiti wa aina hii ili kuinufaisha fasihi ya Kiswahili kwa jumla.

Tumechagua *Haini* kwa vile imejengwa katika mazingira ya Kigereza. Riwaya hii imetoa mwelekeo mwema na data iliyo na manufaa kwa utafiti huu.

## 1.5 Msingi wa Nadharia

Tangu kuibuka kwa fasihi andishi ya Kiswahili, nadharia kadha wa kadha zimetumiwa katika uhakiki wa kazi za kifasihi. Tukichukulia nadharia za uhakiki kama vyombo vya kuchanganua kazi za kifasihi, inakuwa wazi kwamba, lengo la kutumia nadharia yoyote

ile ni uwezo wa nadharia hiyo kutoa mwelekeo mwafaka wa kuhakiki kazi fulani ya kifasihi· Mawazo haya yametiliwa mkazo na Seldon (1989), akinukuliwa na Mbatiah (1999:20) anayesema kwamba, mhakiki anastahili kufanya uamuzi kwa makini wakati wa kuchagua nadharia ya uhakiki. Anasema:

> *kwa maoni yangu, hatuwezi*
> *kuepuka kufanya uteuzi hasa*
> *tujuapo kwamba, kila nadharia*
> *ina athari zake za kisiasa na*
> *kimaadili. Inatubidi tuchague*
> *mitazamo ambayo huangazia*
> *masuala makuu tunayoyashughulikia*
> (Tafsiri yetu)

Uhakiki wetu unaongozwa na nadharia ya Uhakiki wa Ki-Foucault. Hii ni nadharia mojawapo katika kundi pana la nadharia za kijamii. Wamitila (2002:129) anasema kuwa, nadharia za kijamii, ni nadharia ambazo hujihusisha na masuala ya kijamii, hali inayokumba jamii, matatizo yake na masuluhisho yake. Hizi ndizo nadharia ambazo tunaziita za kisosholojia, kama uhakiki wa ki Marx, uhakiki wa Ki-Foucault, Uhistoria Mpya na kadhalika.

Nadharia hii, inahusishwa na Michel Foucault (1926 – 1984), msomi wa Kifaransa ambaye mawazo yake yamekuwa na athari kubwa katika taaluma mbalimbali. Mtaalamu huyu amechangia pakubwa kwenye taaluma ya saikolojia, historia, isimu, falsafa, nadharia za kifasihi na uhakiki wa kifasihi. Mawazo ya Jeremy Bentham kuhusu gereza yamekuwa na mchango mkubwa katika nadharia hii.

Mihimili mikuu ya nadharia hii ni masuala ya **nguvu, maarifa, adhabu, sheria, uchungulizi[3], kudhibiti na gereza.**

Kiini cha nadharia hii ni juhudi za mapambano ya mtu dhidi ya nguvu za kijamii. Foucault, anaiona jamii kama aina ya uwanja changamano ambapo semi au diskosi mbalimbali hung'ang'ania au hushindania nguvu.

Foucault anaonyesha jinsi watu wanavyodhibitiwa na nguvu katika jamii. Anamwona binadamu kama kiumbe asiyekuwa huru bali kiumbe aliyefungwa pande zote na maamuzi ya kijamii. Wazo hili linajitokeza katika mtazamo wake kuhusu jukumu la gereza katika jamii.

Mtazamo wa Foucault kuhusu nguvu na mamlaka umeangaziwa vyema katika kazi yake *Discipline and Punish: The Birth of the Prison* (1977). Katika kazi hii, Foucault ameonyesha jinsi watu wenye nguvu huitawala na kuidhibiti jamii.

Mawazo ya Foucault, yanadhihirisha upinzani wake dhidi ya sheria katika jamii. Anasema kwamba, serikali hutumia mfumo wa kisheria kuwanyanyasa watu na hii ndiyo sababu watu hutenda uhalifu.

Foucault analiangalia kwa jicho pevu suala la adhabu. Anasema kwamba, adhabu inatumiwa katika jamii kuudhibiti umma. Anachunguza kubadilika kwa adhabu kutoka kwa mwili hadi kwa akili[4]. Anachunguza namna adhabu ilivyobadilika kutoka ile ya

kunyongwa kwa wahalifu na kuadhibiwa hadi kuwatia watu kifungoni. Foucault anatalii historia ya kuadhibiwa kwa wahalifu. Anasema kuwa, katika enzi ya mateso[5], haki ya kuadhibu ilikuwa mikononi mwa mamlaka ya mfalme na wahalifu waliadhibiwa hadharani.

Kuhusu gereza, Foucault anasema kwamba, huu ni mfumo wa kuadhibu ambao umeiathiri jamii nzima. Jinsi gereza huwadhibiti wafungwa, ndivyo jamii inavyowadhibiti watu. Watawala hutumia teknolojia ya kisasa na vyombo mbalimbali vya dola katika kudhibiti maisha ya watawaliwa. Maoni yake ni kuwa, jela haikusudiwi kuondoa uhalifu bali kuunda jamii ya watu wanaochukuliwa kuwa wahalifu ambao wamefungwa ili wasiwaathiri wengine.

Kuhusu jamii ya kigereza, Foucault anazungumzia jamii ambamo mfumo wa kigereza umekuwa kanuni kuu katika jamii ya kisasa inayotegemea kwa kiasi kikubwa, udhibiti wa mkondo wa mawazo na maarifa ya wanaotawaliwa na nguvu hiyo. Foucault analinganisha gereza na shule, makao ya wanajeshi na hospitali ambapo mawazo yanadhibitiwa kwa njia moja au nyingine.

Wamitila (2002:172) akiifafanua nadharia hii, anasema kuwa, Foucault anaelekea kuushambulia mwelekeo wa wahakiki wanaotegemea dhamira au lengo la mwandishi kama msingi wa kuzihakiki kazi za fasihi. Badala yake, anawahimiza wahakiki waichunguze mipangilio ya kimaana na ya kitathmini katika kazi za fasihi zinazohusika. Wahakiki wanapaswa pia kuchunguza na kutambua kuwepo kwa mwingilianomatini katika

kazi za fasihi na kazi nyingine, ziwe za kifasihi au la. Kwa maoni yake, shughuli za uhakiki haziwezi kutengwa na maeneo mengine ya maarifa katika jamii. Mawazo haya ni muhimu kwa kuwa yanatuwesheza kuwa na mwanda wa ulinganishi wa kazi mbalimbali na kazi tunayoihakiki na kwa hivyo, kuielewa vyema zaidi.

Tumeichagua nadharia hii kwa kuwa vipengele vyake muhimu vinafaa utafiti wetu; kwa sababu, *Haini* imejengwa katika mazingira ya kigereza nayo mawazo ya Foucault yamejengwa katika misingi ya gereza. Tunaangazia vipengele vyake muhimu na kuonyesha jinsi vinavyodhihirika na kuendelezwa katika *Haini.*

Tunachunguza jinsi suala la nguvu linavyojitokeza katika *Haini*, tunachunguza namna watawala wavyotumia mamlaka yao na sheria kuukandamiza umma, kwa mujibu wa madai ya Foucault. Nadharia hii inatusaidia kuchunguza jinsi wahalifu huadhibiwa katika jamii anayoiandikia mwandishi na kwa jumla, inatusadia kuchunguza iwapo jamii anayoiandikia mwandishi ni jamii yenye mwelekeo wa kigereza.

## 1.6 Upeo na Mipaka

Utafiti wetu umejikita katika uhakiki wa *Haini* riwaya ya Adam Shafi. Ingawaje tumejifunga katika kazi ya mwandishi huyu, tumeyachukua mawazo ya waandishi wengine wanaolandana kimaudhui na msanii wetu kwa lengo la kutilia mawazo yetu mkazo.

Katika utafiti huu tunafanya uhakiki wa kimaudhui. Lakini kwa vile pana mwingiliano mkubwa baina ya maudhui na fani, hatuna budi kupenya katika fani pale ambapo

inalazimu ili kufanikisha uhakiki huu. Mada yetu inaonyesha kwamba, tunachunguza namna taswira ya gereza inavyotumiwa kuendeleza maudhui katika riwaya hii. Katika utafiti huu tunachunguza maudhui ya jamii ya kigereza tu, yanavyosawiriwa na kuendelezwa.

## 1.7 Yaliyoandikwa kuhusu somo

Mpaka sasa hakujatokea tahakiki zozote ambazo zinachambua mada yetu kwa njia ya moja kwa moja. Suala la jamii ya kigereza katika nathari za fasihi ya Kiswahili halijashughulikiwa. Vilevile nadharia ya Ki-Foucault haijatumiwa kuhakiki kazi ya *Haini*. Hata hivyo, zipo kazi zinazoshughulikia uhakiki wa maudhui ambazo zimetufaa kwa kutupa mwelekeo katika kushughulikia mada yetu. Vilevile, zipo kazi ambazo zimehakiki maandishi mengine ya Shafi ambazo zimetufaa katika uhakiki wetu.

Mirieri (1993), ameshughulikia suala la kifo katika uendelezaji wa maudhui katika riwaya ya Kiswahili. Amefanya uhakiki katika kazi mbili za Shafi Adam: *Kasri ya Mwinyi Fuad* (1978) na *Kuli* (1979). Pia ameshughulikia kazi mbili za Muhamed Suleiman Muhamed: *Kiu* (1972) na *Nyota ya Rehema* (1979). Katika uhakiki wake ametumia nadharia ya uyakinifu wa kijamii. Kazi hii imenufaisha uhakiki wetu kwa kuwa imepanua mawazo yetu kuhusu suala la uhakiki wa maudhui.

Sarara (1997) amefanya uhakiki wa maudhui katika tamthilia za Said Ahmed Mohamed. Ingawa kazi hii imejikita katika tamthilia, imetufaa kwa mwelekeo wake wa uchunguzi wa maudhui katika kazi za fasihi.

Njogu (1997) amejishughulisha na maudhui ya mapinduzi katika riwaya za visiwani Zanzibar katika msingi wa nadharia ya uyakinifu wa kijamii. Kazi hii imenufaisha utafiti wetu kwa kuwa sehemu ya kazi hii imejishughulisha na riwaya za Adam Shafi ambaye ni mmoja wa waandishi kutoka Zanzibar. Pamoja na kuwa tunashughulikia riwaya ya Shafi katika utafiti wetu, uhakiki wake umefaa utafiti wetu hasa kwa kuelewa mfumo wa kisiasa, kijamii na kiuchumi nchini Zanzibar na jinsi ulivyowaathiri wandishi wa huko.

Mbatiah (1999) katika "Development of The Swahili Thesis Novel" ameshughulikia suala la maudhui. Pia amegusia kazi mbili za Adam Shafi; *Kuli* na *Kasri ya Mwinyi Fuad.* Kazi hii pia imenufaisha utafiti wetu kwa mwelekeo wa kulishughulikia suala letu.

Kamunde (1983) amejishughulisha na suala la "Kilio cha Wanyonge katika riwaya za Said Ahamed Mohamed". Utafiti wake ni wa kimaudhui; kwa hivyo, umefaa kazi yetu. Aidha kazi yake imefaa utafiti wetu kwa kuwa mada yake inahusiana na yetu kwa njia ya moja kwa moja kwa kuwa, inashughulikia suala la nguvu lililo wazo kuu katika kazi yetu .

Watafiti wengine walioshughulikia suala la maudhui ni pamoja na Mosoti (1993) "Maudhui Katika Tamthilia nne za E. Mbogo", Kitsao (1982) "An Investigation of Themes in Swahili Literature and an Application of Stylostatistics to Chosen Literary Texts", Nekesa (2002) "Treatment of the theme of childhood in Njabulo S. Ndebele's *Fools and other stories"* , Omuteche J. (2004) "Mediated Plot in the Construct of the theme of struggle in Nelson Mandela's autobiography, *Long Walk to Freedom"* .

Umuhimu wa kazi hizi kwa ujumla ni kuwa, zimenufaisha utafiti wetu kwa kutuelekeza jinsi ya kushughulikia maudhui huku tukichunguza na kuangazia namna taswira ya gereza inavyoendeleza maudhui katika riwaya ya *Haini*. Baadhi ya tahakiki tulizozirejelea si za utanzu wa riwaya, lakini zimekuwa muhimu kwetu kwa namna zilivyoshughulikia uchambuzi wa maudhui.

Beiderwell (1992) *Power and Punishment in Scott's Novels,* ametahakiki riwaya za Walter Scott akitumia misingi ya mawazo ya Foucault na yale ya Bentham. Riwaya za Scott anazozirejelea zimejengwa katika masimulizi ya Kigereza ilivyo *Haini.* Katika uchunguzi wake, Beiderwell ameshughulikia, masuala ya adhabu, kulipiza kisasi, haki, nguvu na gereza, katika riwaya hizo. Kazi hii imekuwa msingi na mwelekeo mwafaka katika utafiti wetu.

Pradhan katika, "The politics of power structures" katika Trivedi (1984) amechanganua suala la nguvu linavyodhihirika na kuendelezwa katika riwaya tatu za Joseph Heller: *Catch 22* (1961), *Something Happened* (1974) na *Good as Gold* (1976). Katika uhakiki wake, Pradhan ameshughulikia suala la nguvu kwa namna ambayo imenufaisha utafiti wetu sana.

Maandishi yanayojishughulisha na fasihi ya kifungoni tuliyoyataja katika utangulizi yamekuwa na manufaa kwetu kwa kuwa yametusaidia kuelewa fasihi ya aina hii kwa upana.

## 1.8 Njia za Utafiti

Utafiti wetu umekuwa wa maktabani. Tumesoma kazi ya *Haini*. Pia tumezisoma kazi nyingine za Adam Shafi ili kupata mtazamo wake wa kiitikadi. Aidha tumesoma makala na kazi mbalimbali zinazohusiana na fasihi ya kifungoni. Tumevisoma vitabu vilivyoandikwa na Michel Foucault pamoja na vitabu na makala mbalimbali yanayohakiki kazi za Foucault.

Tumekuwa na mijadala na wataalamu mbalimbali wa fasihi ya Kiswahili.

Vilevile tumetalii mtandao ili kusoma na kuchunguza yaliyo muhimu kuhusu kazi za Foucault, historia ya Zanzibar na uhakiki wa fasihi kwa ujumla.

## Tanbihi

1. Tumetumia istlahi hii ya fasihi ya magharibi, kumaanisha fasihi yoyote iliyoandikwa nje ya bara la Afrika.
2. Taz, Wafula, *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo yake,* Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi, 1999, Sehemu ya utangulizi (ix).
3. Istlahi hii ya uchungulizi tumeizua kutoka kwa kitenzi chungulia. Hii ni hali ambapo, serikali hutumia mbinu mbalimbali katika kuchungulia,kuchunguza na kudhibiti maisha ya wananchi.
4. Enzi ya mateso, inavyoelezwa na Foucault, inarejelea karne ya 18 kule Ulaya wakati washukiwa wa uhalifu waliadhibiwa hadharani. Katika *Discipline and Punish* (1977), Foucault ameanza kwa kueleza jinsi washukiwa walivyoteswa hadharani.
5. Foucault anaieleza adhabu ya kimwili kuwa ni mateso. Nayo adhabu ya kiakili ni adhabu inayotokana na kudhibitiwa kwa watu, hivyo ni akili inayoadhibiwa.

# SURA YA PILI

# MISINGI YA UHAKIKI

## 2.0 Utangulizi

Sura hii imeweka msingi wa yale yanayoshughulikiwa katika utafiti huu. Katika sura hii tumetoa maelezo ya dhana muhimu. Dhana ambazo tumezieleza ni zile zilizomulikwa katika mada yetu: taswira, maudhui na gereza. Tumeeleza maana ya dhana hizi kulingana na jinsi tunavyozitumia katika utafiti huu. Kwa kuwa tunachunguza maudhui ya jamii ya kigereza katika riwaya ya Adam Shafi ya *Haini,* dhana ya jamii ya kigereza kwa mujibu wa mawazo ya Foucault imefafanuliwa. Kama ambavyo kumetajwa kwingine katika kazi hii, uhusiano baina ya fasihi na jamii ni mkubwa, kuelewa mazingira ya kijamii inamokulia kazi fulani ya kifasihi ni hatua muhimu katika uhakiki wa kazi hiyo. Kwa hivyo, katika sura hii kwa muhtasari, tumechunguza mazingira ya kiuchumi, kijamii na kisiasa yaliyoathiri uandishi wa riwaya ya *Haini* ya Adam Shafi.

Kwa muhtasari, sura hii imelenga kutoa mwelekeo kwa utafiti wetu kwa kueleza, tunaelewa na kutumia vipi dhana za taswira ya gereza, jamii ya kigereza na maelezo ya kijumla kuhusu *Haini* na mazingira yaliyoathiri uandishi wa kazi hii.

## 2.1 Dhana ya Taswira

Tumejumuisha sehemu hii katika utafiti wetu katika misingi ya madai kwamba, moja katika matatizo yanayowakumba wasomi na wahakiki wa fasihi ya Kiswahili ni istilahi za kuelezea dhana za kifasihi. Hili ni dai ambalo hatungependa kuliendeleza kwa mjadala,

lakini muhimu ni kwamba, tunataka kuonyesha kuwa, tunapotumia istilahi fulani tunamaanisha nini katika utafiti wetu.

Wamitila (2003:225) anaeleza kuwa taswira ni dhana inayotumiwa kuelezea neno, kirai au maelezo ambayo yanaunda picha fulani katika akili ya msomaji. Taswira zinaweza kuwa za kimaelezo (yaani maelezo fulani yakaunda picha) au za kiishara (zinazounda picha fulani ambayo inaashiria jambo fulani au imeficha ujumbe mwingine). Taswira huweza kuundwa kwa matumizi ya tamathali za usemi hasa tashbihi au sitiari. Ingawa mara nyingi taswira nyingi ni za uoni, panawezekana pakawa na taswira za aina nyingine. Nayo sitiari anaieleza kuwa, ni tamathali ya usemi ielezayo sifa za kitu fulani kwa kusema kuwa ni za kingine. Hii ni mbinu ya kulinganisha kama tashbihi, lakini ulinganishaji huo haujitokezi waziwazi. Sitiari huhusisha vitu viwili ambavyo ni tofauti kitabia na kimaumbile. Katika msingi huu, tunaweza kusema kuwa sitiari, kama zilivyo tamathali nyingi imejengeka kwenye uhamishaji wa maana ya kisemantiki. Matumizi ya sitiari yanaweza kuwa yanalenga hisia au fahiwa (kirejelewa) fulani au kujenga picha au taswira fulani. Kwa mfano, unapomwita mtu fulani "nguruwe", inawezekana ikawa mtu anayehusika ana sifa kadhaa zinazofanana na za mnyama huyo, kama ulafi au ukoo (uchafu). Pia inawezekana kwamba, hisia zako kwake ni kama hisia ulizo nazo kila umwonapo mnyama huyo.

Kuna aina nyingi za taswira na vilevile aina nyingi za sitiari. Kwa lengo la utafiti wetu, tunachukua jukumu la kueleza taswira kuu ambayo kwa mujibu wa Wamitila. (k.h.j.), ni sawa na sitiari kuu. Hii ni dhana inayotumiwa kueleza taswira au sitiari inayochukua nafasi kuu katika kazi za kifasihi. Taswira au sitiari ya aina hii, huwa na uhusiano mkubwa na

maudhui ya kazi inayohusika. Mifano ni safari katika *Nagona* na *Mzingile,* riwaya za . Kezilahabi na gereza katika *Haini.*

Mbatiah (2001:25) anasema kuwa, taswira pia huitwa jazanda. Maelezo yake ya jazanda / taswira ni kuwa, ni kunga ya utunzi inayotumiwa kusawiri picha fulani. Hii inatokana na maelezo yanayotumia maneno mateule au tamathali za usemi. Kwa njia hii, mtunzi anamwezesha msomaji kuona, kuhisi au kunusa kinachoelezwa. Mtaalamu huyu anasema kuwa, taswira/jazanda hujengwa kwa matumizi ya tamathali za usemi kama vile tashbihi na sitiari. Sitiari anaieleza kuwa ni tamathali inayotumia ulinganishi ambapo vitu viwili ambavyo ni tofauti kitabia na kimaumbile, vinahusishwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Lengo la sitiari ni kuonyesha udhahiri na msisitizo katika maelezo.

*Encyclopedia Americana* (1977:196.vol. 11) inaeleza sitiari kuwa ni ulinganisho wa vitu viwili visivyofanana. Ulinganisho ambao kimawazo hufananisha sifa za kitu kimoja kwa kile kingine kinacholinganishwa nacho. Sitiari hutumiwa na wazungumzaji au waandishi kwa hiari au kisanaa, ili kufanikisha mawasiliano au kwa lengo la kusisitiza.

Sitiari/taswira/jazanda ni tamathali za usemi. Tamathali za usemi ni mbinu ya kujieleza ambayo hutumia maneno kwa njia isiyo ya kawaida ili kufanikisha athari fulani. Kwa mujibu wa Ensaiklopidia hii,hakujatokea mfumo wa kutosheleza wa kuainisha tamathali za usemi kwa kuwa; ni nyingi , zina uhusiano wa karibu sana na zinaingiliana kwa kiwango kikubwa.Kwa mujibu wa utafiti wetu ,tumechukulia taswira/jazanda kwa maana ya sitiari.

Matumizi ya jazanda ni moja ya sifa muhimu katika fasihi ya Kiswahili. Kwa mfano, katika tamthilia za; *Wingu Jeusi* (1987) ya Nyaigoti, *Kivuli Kinaishi* (1990) ya Mohamed na *Mashetani* (1971) ya Hussein , mbinu hii inajitokeza. Wafula. (1999: 124) anasema kwamba, katika *Wingu Jeusi,* mwandishi anaiajiri jazanda ya Wachinato kusuta maovu ya kisiasa na kijamii yanayofanywa na viongozi wa Kiafrika. *Kivuli Kinaishi*, ni tamthilia inayoshirikisha ngano ya miviga ya kuwaingiza wanajamii jandoni kwa minaajili ya kuonyesha tasnifu ya udikteta na ukombozi. Katika *Mashetani,* shetani ni jazanda inayotumiwa kuonyesha viwango mbalimbali vya uharibifu unaotendeka katika jamii za kiafrika. Vivyo hivyo, katika *Haini,* gereza ni jazanda inayoonyesha namna maisha ya jamii zetu yalivyo na ufanano na gereza.

## 2.2 Maudhui

Maudhui ni jumla ya mambo yanayozungumziwa na kukuzwa katika kazi ya kifasihi. Ni muhimu kutaja kuwa, kazi yoyote ya kifasihi huwa na maudhui mengi. Wahakiki mbalimbali wanaweza kutofautiana au kuafikiana kuhusu maudhui yaliyo katika kazi fulani. Hii hutegemea mikabala, vipengele na malengo yao, katika kuchunguza maudhui katika kazi hiyo. Kwa mtazamo wa nadharia ya Ki-Foucault, utafiti wetu unachunguza namna maudhui ya jamii ya Kigereza yanavyosawiriwa na kuendelezwa katika viwango mbalimbali, katika riwaya ya *Haini.*

## 2.3 Gereza na Jamii ya Kigereza

Gereza ni moja ya mbinu kuu za kuadhibu inayotumiwa ulimwenguni kote. Kila siku, vyombo vya habari kote ulimenguni hutoa habari inayohusu uhalifu na kifungo. Kazi za utanzu wa fasihi ya kifungoni zimejaa masimulizi kuhusu hali na maisha ya gerezani.

Ni muhimu katika kiwango hiki kufafanua dhana ya gereza na jamii ya kigereza. *Encyclopedia Americana* (1977:619:vol. 22) inaeleza gereza kuwa ni mahali washukiwa wa uhalifu wanamofungiwa wakingojea kufikishwa mahakamani, au ni mahali wahalifu hufungiwa kama njia ya kuwaadhibu. Katika historia ya binadamu, jela zimekuwepo tangu azali; zamani zikitumiwa tu kama mahali pa kuwafungia washukiwa wakingojea hukumu. Matumizi ya jela kama njia ya kuadhibu wafungwa si jambo lililo na historia ndefu. Katika Ulaya na Marekani, jela zilianza kutumiwa rasmi kama njia ya kuadhibu mnamo miaka ya mwanzo ya karne ya 19.

Kwa mujibu wa Ensaiklopidia hii, jela hutekeleza majukumu matatu makuu: kuadhibu, kufungia na kudhibiti. Wahalifu au washukiwa wa uhalifu hufungiwa kama njia ya kuwaadhibu na wakati huo huo huwa ni njia ya kuwadhibiti. Ensaikloipidia hii inadokeza kuwa, jela ni kioo cha ulimwengu na wa nje (jamii iliyo nje ya gereza), kwa kiasi fulani.

Encyclopedia ya *New Universal Library* (1967:193 vol 11) inaafikiana na *Encyclopedia Americana (k.h.j.)* kuhusu fasiri ya gereza pia inaeleza kuwa, watawala wamezidumisha jela tangu zamani zikiwa mahali pa kuwafungia washukiwa wakingojea hukumu. Aidha nayo inaeleza kwamba, jela kama njia ya kuadhibu sio jambo lililo na historia ndefu.

Jambo lililo wazi ni kuwa, katika ulimwengu wa leo, jela ni mahali pa kuwafungia washukiwa wakingojea hukumu au kama njia ya kuwaadhibu wahalifu. Hili ndilo jukumu tunaloona jela ikitekeleza katika *Haini* na katika kazi nyingine za fasihi ya kifungoni. Katika *Haini,* Hamza na wenzake wamekamatwa na kurundikwa gerezani. Wanabaki gerezani kwa jumla ya miaka miwili hadi mahakama inapotoa uamuzi kuhusu kuhusika au kutohusika kwao. Hamza na baadhi ya wenzake wanaachiliwa huru kwa ukosefu wa ushahidi wa kuwahusisha na mauaji ya Kigogo. Baadhi ya wale washukiwa wanahukumiwa kifo na wengine wanahukumiwa kifungo cha miaka kumi na mitano kama njia ya kuwaadhibu.

Gereza ni moja ya asasi katika jamii ambazo zimetoa mchango katika kuendeleza fasihi kimaudhui. Imebainika kwamba, waandishi wengi wa fasihi ya kifungoni, katika kipindi kimoja au kingine walilwahi kufungwa gerezani. Waandishi hawa wametumia tajriba zao za gerezani katika uandishi wa kazi za fasihi. Namna ambavyo wanavyojenga taswira za gereza zinazodhihirika katika kazi za aina hii, ni mambo ambayo msanii asiyekuwa na tajriba ya kifungoni hataweza kuyaeleza sawa na aliyefungwa.

Kwa mujibu wa Focault (1973) dhana ya kifungo ina historia ndefu. Dreyfus na Rabino (1982) wanasema kwamba, katika *Madness and Civilisation* (1973), Foucault anaiangalia historia ya kifungo kuanzia Enzi ya Kati huko Ulaya. Katika enzi hii, wagonjwa wa ukoma walifungiwa katika nyumba maalum zilizokuwa katika kingo za miji ya Ulaya. Katika Enzi ya Muamko wa Sanaa wendawazimu walirundikwa melini na kuachiliwa kuabiri kufuata

mikondo ya mito ya Ulaya. Wenda wazimu wakawa wafungwa katika ulimwengu huru. Katika karne ya 17, makazi ya kuwafungia wagonjwa wa ukoma yakafanywa mahali pa kuwafungia maskini.

Foucault anaeleza kuwa, haja ya gereza ilizuka kama njia ya kuadhibu. Katika *Discipline and Punish: The Birth of the Prison* (1977) Focault anatalii kubadilika kwa adhabu kutoka mateso ya hadharani hadi kufungiwa kwa wahalifu. Awali, katika enzi anayoiita "Enzi ya Mateso", washukiwa waliteswa hadharani kwa amri ya mfalme kwani kila kosa lilichukuliwa kuwa kosa dhidi ya mfalme. Kuelekea mwisho wa karne ya 18, watu walipinga mateso ya hadharani kwa washukiwa jambo lililopelekea kuanzishwa kwa gereza kama njia ya kaudhibu. Kuwanyima watu uhuru kwa kuwafungia, kulionekana kuwa njia iliyoleta usawa katika kuwaadhibu washukiwa.

Mbali na kuwanyima watu uhuru, jela ziliendelea kuwa mahali pa kuadhibu kwa kuumiza. Adhabu ilikusudiwa kuwafanya wahalifu wawe wanajamii wema wafunguliwapo kutoka gerezani. Alper (1974:9) anasema kuwa, mitindo ya magereza ya kisasa ya kuwafungia wahalifu na kuwafanyisha

kazi ngumu ili kuwarekebisha tabia, ni mambo yaliyonuiwa kuchukua nafasi ya mitindo ya zamani ya kuadhibu, Lakini njia ya mateso imejumlishwa katika magereza ya kisasa. Kazi za utanzu wa fasihi ya kifungoni zilizoandikwa katika mazingira ya kiafrika, masimulizi ni yale yale mateso. Katika *Never Say Die (1998)* Kihoro anaeleza anavyoteswa na Askari kanzu wa Kenya katika vyumba vya mateso akiwa kifungoni. Kinyatti katika *Kenya: A prison Diary (*1996*)* ana masimulizi sawa ya mateso kwa njia ya kuumiza mwili.

Baada ya kutembelea magereza katika nchi za Ufaransa na Marekani, Foucault anahitimisha kwamba, mbinu za kisasa za kuadhibu ni mbaya zaidi kuliko zilivyokuwa zile za awali. Katika *Discipline and Punish* (1977), Foucault anaushambulia mfumo wa kigereza kwa kuwa ni mfumo ulioshindwa kutekeleza majukumu yake. Kulingana naye, lengo kuu la jela lilikuwa kupunguza uhalifu kwa kuwaadhibu washukiwa, kwa hivyo kuwazuia wengine kushiriki katika matendo ya uhalifu.Foucault (k.h.j:267) anasema:

> *Jela hazipunguzi matukio ya uhalifu. idadi ya wahalifu hubakia au huongezeka. Kuzuia wafungwa kunawafanya sugu; wale wanaoachiliwa kutoka jela wana nafasi kumbwa ya kurudi huko. Jela hufaulu kuongeza na kutengeneza wahalifu kwa mbinu zake za kuadhibu.*
>
> (Tafsiri yetu.)

Mbali na kuwa jela zimeshindwa kutekeleza malengo yake, Foucault anasema kwamba, mfumo huu umestawi kwa sababu unawanufaisha watawala; watawala wanatumia jela kuwafungia wahalifu, kama njia ya kuzuia maasi. Wazo kuu analolitoa hapa ni kuwa, jela au gereza havikusudiwi kuondoa uhalifu bali kuunda jamii ya watu wanaochukuliwa kuwa "wahalifu" ambao wamewekwa kwa njia isiyowaathiri wengine au isiyo kuwa nzito kiuchumi.

Watawala hutumia sheria kama njia moja ya kudhibiti watu hawa. Mfumo wa kisheria unatumiwa kuwatenganisha watu wenye uwezo katika jamii ya watawaliwa kwa hivyo, kupunguza uwezo wao kisiasa. Foucault (k.h.j: 276) anasema:

*Itakuwa unafiki kuamini kuwa sheria iliundwa kwa wote, ni busara kuonyesha kuwa sheria ilitengenezewa wachache kuwakandamiza wengine.*

(Tafsiri yetu)

Sheria zinatumiwa kuwasingizia watu hawa uhalifu na kwa hivyo, kuwadhibiti kwa kuwaweka gerezani. Sheria kama mbinu ya kudhibiti umma, ni sifa inayotawala jamii za kigereza. Kwa mfano, Orwell katika *Shamba la Wanyama* (1967) amesawiri jamii ambamo watawala wanabadilisha sheria ili zikidhi manufaa yao huku zikiumiza umma. Umma unaumizwa chini ya mfumo huo wa sheria kandamizi huku jamii nzima ikiwa kama gereza.

Katika *Discipline and Punish,* Foucault anaonyesha jinsi mfumo huu wa kigereza wa kuadhibu, ulivyoiathiri jamii nzima. Kupanuka huku kwa mfumo wa kuadhibu anakuita 'Bahari ya Kigereza'. Matokeo ya mfumo huu ni kuwa, huzaa jamii tiifu chini ya mamlaka ya watawala.

Mageuzi ya kigereza ya Jeremy Bentham, ni mfano bora wa mawazo ya Foucault kuhusu gereza. Jeremy alipendekeza mnara wa ulinzi[1] uwe muundo wa gereza imara. Alipendekeza muundo wa gereza uwe wa mtindo ambao, vyumba vya wahalifu vitajengwa vikiuzunguka ule mnara. Aliye mnarani huweza kuwaona wote walio vyumbani. Lakini walio vyumbani, hawawezi kumwona aliye mnarani. Wakati wowote mfungwa asingefahamu kuwa analindwa au la, lakini kila mara huwa na imani kuwa yu chini ya ulinzi.

Kuhusu jamii ya kigereza, Foucault anazungumzia jamii ambamo mfumo wa mnara wa ulinzi umekuwa kanuni kuu katika muundo wa jamii. Katika hali hii, muundo huu huchukua jukumu la kudhibiti jamii. Muundo huu ni taswira ya jinsi jamii inavyopaswa kuwa. Ili kuleta utaratibu katika jamii, watu wanastahili kuamini kuwa wanalindwa na kuchunguliwa wakati wote. Katika hali hii, watawala hudhibiti umma kwa kuwa kile chombo cha kuona kipo kila mahali. Mfumo huu wa ulinzi umeendelezwa katika jamii zetu kupitia maendeleo mapya ya teknolojia ambayo yanasaidia mawakala wa serikali kuchunguza mienendo ya watu. Matumizi kama vile ya simu, mtandao wa Intaneti, kamera za ulinzi, na maendeleo mengine ya teknolojia ya kisasa, yameendeleza ulinzi katika jamii zetu.

Foucault analinganisha gereza na viwanda, mashule, makao ya wanajeshi na hospitali. Hizi ni asasi ambazo hudhibiti maisha ya watu kigereza. Asasi zote katika maisha ya jamii za kisasa hudhibiti maisha ya watu yanavyofanya magereza lakini kwa kutumia ujanja. Vyombo hivi vya kuadhibu huzaa watu watiifu, wenye bidii na waaminifu kwa watawala.

Kwa jumla, katika *discipline and Punish,* Foucault haielezi tu historia ya magereza ya kisasa, bali kazi hii inamulika mawazo na diskosi zilizozizaa jamii za kisasa za kigereza. Foucault anauona mfumo wa kigereza kama unaoliwezesha tabaka la watawala kukandamiza tabaka la watawaliwa. Mfumo huu hutekeleza malengo yake kwa kuwafungia, kuwatenganisha na kuwakandamiza wanajamii wenye uwezo katika tabaka la watawaliwa; kulifanyia hivi kundi hili, hupunguza uwezo wake wa kisiasa na kijamii. Mfumo wa kigereza wa kuadhibu umeenea katika jamii nzima. Watu wanaopambana dhidi

ya mfumo huu wa kuadhibu huitwa 'wahalifu', kuna pia wale wanaoutii na kupoteza kitambulisho chao ambao kwa Foucault, ndio huwa wahalifu hasa.

Kwa muhtasari, jamii ya kigereza ni jamii inayolanda gereza kimwelekeo; ni jamii ambamo watawala hutumia uwezo wa dola kwa njia rasmi kudhibiti umma, sheria hutumiwa kwa manfuaa ya wachache, vyombo vya dola hutumiwa kudhibiti na kukandamiza umma; kiuchumi, kijamii na kisiasa umma hufungwa kigereza. Mfumo huu husababisha kujitokeza kwa jamii inayotawaliwa na hofu, usaliti, kutoaminiana, unafiki na mateso ya hali ya juu kwa wanajamii wengi.

Utafiti huu umetuwezesha kuelewa mfumo mzima wa jamii pana kwa kuchunguza gereza. Lakini ieleweke sio matukio yote ya gerezani yaliyo kioo cha jamii pana, pana na ufanano na tofauti pia.

## 2.4 *Haini*: Mazingira ya Kisiasa, Kijamii na Kiuchumi

*Haini* ni riwaya iliyoandikwa na Adam Shafi. Takribani riwaya zote za Shafi ni za kihisotria. Riwaya ya kihistoria huchukua tukio au matukio fulani ya kihistoria au hata mhusika fulani na kumfanya kiini cha riwaya yenyewe. Riwaya za *Kuli* (1979) *na Kasri ya Mwinyi Fuad* (1978), zinaakisi kwa kiasi kikubwa maudhui ya mapinduzi kisiwani Zanzibar yaliyotokea mnamo mwaka wa 1964. Mapinduzi haya yaliondolea mbali utawala wa kisultani na kubadili kwa kiasi kikubwa, mfumo wa uzalishaji mali visiwani humo.

*Haini* pia inaakisi tukio la kihistoria – kuuawa kwa Rais wa Zanzibar Abeid Amani Karume mnamo mwaka wa 1972. Watu wengi wasiokuwa na hatia walisakwa na kukamatwa na kutiwa gerezani kwa kutuhumiwa kuwa mahaini. Mwandishi amelitumia tukio hili kuwa kiini cha kuyachunguza matatizo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii ya nchi za Kiafrika baada ya uhuru.

Kwa kile ambacho tunakiita uandishi wa historia kisanaa, kwa ufundi mkubwa mwandishi ameliwasilisha tukio hilo kisanaa. Ni vizuri ikumbukwe kuwa, lengo la utafiti huu si kuchunguza historia ya tukio hili kama linavyowasilishwa kisanaa. Hili linatajwa kwa kuwa ni msingi muhimu katika suala tunalolichunguza la jamii ya kigereza. Hii inatokana na sababu kuwa, ni muhimu kwa mhakiki yeyote na hasa mhakiki anayechunguza kazi ya kifasihi katika misingi ya mojawapo ya nadharia za kijamii, kuielewa jamii anayoichunguza. Oladele (1982:2) akinukuliwa na Mbatiah (1999:22) anasema kuwa, wahakiki wengi wa kigeni hufanya makosa katika kuzihukumu kazi za kifasihi za kiafrika, kwa sababu ya kutoelewa mazingira ya kijamii, kisiasa na kijamii kazi hizi zinamokulia. Anasema:

> *Kwa mhakiki wa kiafrika kuweza kufaulu katika kazi yake, katika maandalizi yake ya kijumla, anahitaji kufahamu desturi, maarifa, utamaduni na mabadiliko katika mazingira ya watu wa jamii iliyoandikiwa.*
>
> (Tafsiri yetu)

Hii ndiyo sababu imekuwa muhimu kwetu, kwanza kuelewa mfumo wa kisiasa, kijamii na kiuchumi wa kisiwa cha Zanzibar, ambayo ni jamii anayoiandikia Adam Shafi.

Zanzibar ni muungano wa visiwa viwili, Unguja na Pemba, vilivyo mkabala na Tanzania bara katika Bahari Hindi. Data ya historia inaonyesha kwamba, kufikia karne ya 15 Zanzibar ilikuwa kituo muhimu cha kibiashara kati ya Afrika, Mashariki ya Kati na India. Mnamo mwaka 1503, Wareno walivamia Zanzibar na kuanzisha utawala wao huko. Waarabu kutoka Omani waliwaondoa Wareno utawalani mnamo mwaka 1698. Mnamo mwaka 1832, Sultani Sayyid Said wa Omani alihamisha makao makuu yake hadi Zanzibar. Wakati wa enzi ya ukoloni barani Afrika, mkataba wa Waingereza na Wajerumani wa mwaka 1890 uliifanya Zanzibar koloni la Waingereza lakini ikitawaliwa na Sultani, hali iliyoendelea hadi mwisho wa Vita vya Pili vya Dunia.

Mfumo wa kisiasa na kiuchumi ulioimarishwa na Waarabu nchini Zanzibar, unaweza kuelezwa kuwa ulikuwa wa kikabaila. Serikali iliongozwa na sultani na tabaka la watawala ndilo lilimiliki mashamba na watumwa. Kuwepo kwa Waingereza, kulibadilisha mfumo wa kiuchumi kuwa wa kibepari.

Mnamo tarehe 10/12/1963 Uingereza ikaipa Zanzibar Uhuru chini ya uongozi wa Sultani. Kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964, Zanzibar ilikuwa jamii yenye mfumo wa kitabaka; kulikuwa na tabaka la Waafrika maskini waliokuwa wengi; Wahindi –wafanyi biashara; na Waarabu-watawala na wamiliki mashamba.

Kiuchumi, Zanzibar ilitegemea ukuzaji wa nazi na karafuu katika mashamba makubwa yaliyomilikiwa na Waarabu. Waafrika walikuwa watumwa na wapagazi katika mashamba

haya. Muundo huu wa kitabaka na Kiuchumi uliowanyanyasa waafrika, ndio ulisababisha mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.

Haya ndiyo maudhui yanayotawala katika kazi nyingi za waandishi wa Zanzibar kama vile ya Mohamed Suleiman Mohamed na Adam Shafi. Katika mapinduzi haya, utawala wa Sultani uling'olewa na waafrika walio wengi, Zanzibar ikawa Jamhuri chini ya uongozi wa Abeid Amani Karume. Katika *Haini,* mwandishi anamulika historia hii ya Zanzibar kutoka mbali anaposawiri sifa za Chopra, mwendesha mashtaka wa serikali. Anasema:

> *Jinsi alivyokuwa bingwa wa kazi yake hiyo, aliaminiwa sana na mahasimu wote watatu waliokitawala kisiwa cha Zanzibar. Wakati wa Elizabeth wa pili aliaminiwa sana na watawala wa kiingereza na utiifu wake kwa watawala hao ukawa ni wa kupigiwa mfano. Sultani na wafuasi wake walipofanikiwa kuundoa utawala wa Elizabeth wa pili na kuweka utawala wao, nao pia wakawa na imani kubwa na Chopra wakamfanya kuwa ndiye mshauri wao mkuu wa mambo ya kisheria ...wakwezi na wakulima walipokuja juu wakamtimua Sultani na wafuasi wake kwa mapanga na mashoka na Kigogo akashika usukani wa kuiongoza nchi, Kigogo hakumwona mwanasheria aliyekuwa na kipawa kumshinda Chopra, akampandika cheo cha mwanasheria mkuu wa serikali.*
> *(uk 230 – 231)*

Abeid Amani Karume aliuawa mnamo mwaka 1972. Taifa la Zanzibar likashuhudia kilele cha ukiukaji wa haki za kibinadamu katika kile watawala walichokiita 'usakaji wa mahaini', wauaji wa Karume. Watu wengi waliteswa, wengi wakauwawa na wengi walifungwa gerezani kwa shutuma za kushiriki mauaji ya Karume. Taifa likawa kama gereza. Hili ndilo tukio ambalo Shafi analimulika katika *Haini.*

Historia hii ya Zanzibar, imeonyesha desturi ndefu ya kunyanyaswa kwa umma katika tawala mbalimbali ambazo zimedhihirisha mfumo wa utawala unaojali maslahi ya watawala wachache,huku watawaliwa walio wengi wakiumia. Ni historia ambayo imedhihirisha matumizi ya nguvu rasmi, katika kuwakandamiza na kuwadhibiti watawaliwa. Hali hii inaendelezwa katika Zanzibar huru, jamii ambayo Shafi anaizungumzia katika *Haini.*

## 2.5 Muhtasari wa *Haini*

Kwa muhtasari, *Haini* ni riwaya inayozungumzia matukio katika taifa la Zanzibar baada ya majaribio ya kuipindua serikali, machafuko ambayo yanasababisha kuuawa kwa kiongozi wa nchi Mheshimiwa Kigogo. Raia wengi wanakamatwa kwa kuhutumiwa kuwa mahaini. Mmoja wa watuhumiwa hao ni Hamza, kijana mwandishi wa habari ambaye anakamatwa kwa sababu ya usuhuba wake na Hamduni ambaye amempiga risasi na kumwua Kigogo.

Riwaya inatufungulia milango ya mazingira yaliyojaa hofu na wasiwasi. Raia wanasakwa, kukamatwa na kutiwa gerezani kwa kosa ambalo wengi wao hawalifahamu. Sehemu kubwa ya riwaya hii, inasimulia matukio ya gerezani ambamo Hamza pamoja na watuhumiwa wengine wamerundikwa, kuteswa, kuthakilishwa na kutendewa unyama wa kila aina.

Hamza na wenzake hawana budi kuumia huku wakiwa hawajui hatima yao. Wanateswa ili wakiri kwamba walihusika. Baadhi yao hawana budi kufanya hivyo ili kuokoa roho zao. Mkadam, Haramia, Mpakani, Sumbu, Marzuku, Vingosho, Zarkani, Pwacha na Kuchi wanakiri kuhusika kwao. Wanatungiwa visa na ushahidi wa uwongo wa kuwahusisha wale wengine.

Hatimaye, "mahaini" wanapofikishwa mahakamani kujibu kesi ya jinai nambari mia mbili na ishirini na tano, Hamza na baadhi ya wenzake kama Faraji hawapatikani na hatia kwa hivyo wanaachiliwa huru. Mkadam na wenzake wanaokiri kuhusika, wanahukumiwa kifo. Kundi jingine kama la Sururu na Ambar, wanahukumiwa miaka kumi na mitano kila mmoja kwa kosa la kutowaarifu polisi juu ya mpango wa uhaini ambao wao waliiujua, ijapokuwa hawakushiriki.

Ingawa masimulizi mengi ni ya matukio ya gerezani. Mara moja moja mwandishi hututoa nje na kumulika hali ya wasiwasi na hofu inayotawala jamii pana, pamoja na mateso yanayowakumba wake wa "mahaini" na familia zao hasa Khadija mkewe Hamza.

Hatimaye Hamza anafunguliwa kutoka gerezani na huu ndio mwisho wa riwaya. Tunasoma:

> *Alitoka nje ya lile gereza kwa kupitia kwenye kilango kidogo kilichotobolewa kwenye lile lango kubwa. Alipofika nje akasimama, akaliangalia jua, kali linawaka kama moto. Akavuta hewa na pale aliposimama, hewa safi kabisa hainuki uvundo wa mitondoo wala kupuo la uchafu wa vyumba vya gereza lile. Yuko huru, akamkumbuka Abdul,*

*akayakumbuka na maneno yake, "tutatoka tu!" kweli ametoka.*

*"Na hao waliobaki, nao pia watatoka tu," alisema Hamza. Yuko peke yake. Aligeuka nyuma kuliangalia lile lango la gereza. Alilitazama kwa chuki na hasira, uchungu ukamjaa moyoni akawaza jinsi lango lile lilivyoficha nyuma yake mateso na madhila.*
*(uk. 267)*

## 2.6 Hitimisho

Sura hii imeweka msingi ambao ni muhimu katika utafiti huu. Dhana za taswira/sitiari na maudhui zimefafanuliwa. Tumeonyesha namna dhana za taswira na sitiari zilivyofafanuliwa na baadhi ya wataalamu wa fasihi, nasi tumeonyesha namna tunavyozitumia katika utafiti huu. Sura hii, aidha imefafanua dhana za gereza na jamii ya kigereza. Tumeeleza maana na majukumu ya gereza kama asasi ya kijamii ambayo athari zake zimeonekana katika kazi nyingi za fasihi. Tumeonyesha namna Foucault anavyoiona dhana ya gereza na jamii ya kigereza, kwa mujibu wa kazi yake ya *Discipline and Punish (1977)*. Mjadala huu umeliwekea suala la jamii ya kigereza msingi imara kwa kuwa ndilo tunalishughulikia katika utafiti huu.

Tumeangazia historia ya Zanzibar kwa muhtasari kwa kuwa tumeafikiana na asemavyo Oladele (1982) kwamba, ni muhimu kwa mhakiki yeyote kwanza kuelewa jamii inayozungumziwa katika kazi ya fasihi, kama hatua muhimu na ya kimsingi ili tunapozihukumu kazi za kifasihi tuwe na mashiko.

**Tanbihi.**

1. Mnara wa ulinzi – ni mnara ambao unajengwa gerezani, ambapo askari huwa, ili kuwachungulia wafungwa. Mnara huu, pia tumeuita 'mnara wa uchungulizi' katika utafiti huu.
2. Tumetumia istlahi ya jamii pana kumaanisha jamii iliyo nje ya gereza. Jamii ambamo magereza yamejengwa.

# SURA YA TATU

# MAUDHUI YA JAMII YA KIGEREZA KATIKA *HAINI*

## 3.0 Utangulizi

Katika sura hii, tunachunguza namna maudhui ya jamii ya Kigereza yanavyosawiriwa na kuendelezwa katika *Haini.* Kwa kufanya hivi, tunafafanua namna sifa za jamii ya Kigereza kwa mujibu wa nadharia ya Ki-foucault zinavyosawiriwa na kuendelezwa katika riwaya hii. Tunachunguza viwango mbalimbali vya usawiri wa maudhui haya.

Kabla ya kuukweza mjadala wetu katika ngazi ya yale tunayolenga kuyachunguza, hatuna budi kulishughulikia suala la 'uhaini' kwa kuwa ndilo limeweka msingi wa suala tunalolitafiti. Kichwa cha riwaya, 'Haini' kinatuelekeza moja kwa moja kwenye suala linalozungumziwa katika riwaya hii. Kwa mujibu wa kamusi ya Kiswahili Sanifu, 'haini' ni mtu anayesaliti nchi, serikali au mfadhili wake. Inaendelea kumweleza kuwa ni mshiriki katika jambo baya; mdanganyifu, mtoro, msaliti au mwasi.

Katika *Haini,* kunatekelezwa majaribio ya kuiangusha serikali, machafuko ambayo yanasababisha kuuawa kwa kiongozi wa nchi, Mheshimiwa Kigogo. Njama hii inapangwa na viongozi wakuu serikalini na jeshini. Kanali Bunju na Kubwalao ndio viongozi wanaohusika. Kwa mujibu wa Haramia, mshukiwa wa uhaini ambaye alikuwa mtu wa karibu na kanali Bunju, Kanali Bunju ni mmoja wa waasisi wa mpango huo. Naye Mkadam anaamini mwasisi wa mpango huo ni Kubwalao.

Baada ya mauaji ya Kigogo, Kanali Bunju anawaua wote waliohusika na mauaji; hakumbakisha hata mmoja. Waliokuwa na fununu kuhusu jukumu lake katika mpango huo kama vile Haramia wanawasokomezwa gerezani. Pamoja na hayo, anaongoza msako wa watuhumiwa wanaosadikiwa kuhusika na mpango huo.

Hamza, kijana mwandishi wa habari na watu wengine wengi, wanajipata kufagiliwa na wimbi kali la tukio hilo na kubatizwa 'mahaini'. Hamza ni rafiki mkubwa wa Hamduni ambaye ameuawa kwa kumpiga risasi na kumwua Kigogo. Watuhumiwa wengine wanakamatwa kwa kuwa majirani wa Hamduni kwa mfano familia ya Edi. Wengine wanakamatwa kwa kushukiwa kwamba, wanasherehekea kifo cha Kigogo, kwa mfano Mzee Subet anayekamatwa kwa sababu anamchinja jogoo wake akisingiziwa kwamba anasherehekea kifo cha Kigogo.

Ukweli ni kwamba, wakuu wa serikali wanafahamu kuhusu mpango huo wa mapinduzi ya serikali na mauji ya Kigogo, kwa hivyo, ndio mahaini hasa. Wanaokamatwa na kusokomezwa gerezani ni watuhumiwa tu ambao wengi wao hawana ufahamu wowote kuhusu uhaini huo. Kanali Bunju na wenzake wanatekeleza haya yote ili kuufunika ukweli na zaidi kama asemavyo Foucault, kwa sababu ya uwezo na nguvu rasmi walizonazo. Uwezo ambao unawawezesha wao viongozi kutumia nguvu zao kuwakandamiza raia wasiokuwa na hatia kwa kuwatia gerezani na kwa hivyo, kuunda jamii ya wahalifu ('mahaini'). Sehemu kubwa ya hadithi ya Haini ni taswira ya gerezani wanamojikuta akina Hamza.

Maudhui ya jamii ya Kigereza yamesawiriwa katika viwango mbalimbali, katika sura hii tumechunguza viwango vitatu vikuu: **Adhabu, nguvu na uangalizi**. Tumevijadili kwa undani na kuvitolea mifano mwafaka kutoka kazi hii tunaiyoichunguza na aidha kutoka kwa kazi nyingine ambazo tumeona zinafaa katika kutilia mawazo yetu msisitizo.

## 3.1 Adhabu

Adhabu ni moja katika masuala makuu yanayozungumziwa na nadharia ya Ki-Foucault. Nadharia hii inaonyesha kuwa, adhabu ni mbinu kuu inayotumiwa na watawala katika kuukandamiza na kwa hivyo, kuudhibiti umma. Viongozi wanatekeleza hili kwa kuwa wana nguvu. Katika *Discipline and Punish* (1977), Foucault amezitalii njia mbili kuu za kuadhibu: gereza na mateso.

### 3.1.1 Gereza

Moja katika sifa kuu za jamii ya Kigereza ni matumizi ya gereza kama njia ya kuadhibu na vilevile athari za mfumo wa kigereza katika jamii pana. Katika *Haini,* kukamatwa na kufungiwa gerezani kwa Hamza na wenzake ndilo tukio muhimu katika riwaya hii, kwani matukio yote yanayosimuliwa yamejengwa katika tajriba za Hamza na wenzake katika mazingira ya kigereza.

Gereza linachukua nafasi muhimu katika riwaya hii sio tu kwa kuwa limetumiwa kistiari,bali pia kwa kuwa ni asasi mojawapo zinazotumiwa na watawala kama chombo cha kuwakandamiza raia. Kwa jumla, jamii anayoiandikia Adam Shafi ni jamii inayotumia gereza (kifungo) na mfumo wa Kigereza katika kuadhibu. Gereza limesawiriwa kwa njia

mbili: kwanza, gereza lenyewe linalotumiwa kuwafungia wahalifu na washukiwa wa uhalifu na vilevile, taifa zima limesawiriwa kama gereza moja kuu kwa jinsi ambavyo limeathiriwa na mfumo wa kigereza.

Mwandishi ametumia gereza kuu la Zanzibar la Kinoamiguu kama kielelezo cha mfumo wa Kigereza katika taifa hilo. Shafi amefaulu kutuchorea picha ya maisha ya gerezani. Amefanya hivi kwa kuwamulika wafungwa, hali zao, maslahi yao, hisia zao, malalamiko na harakati nyingine katika maisha yao ya kila siku gerezani. Katika gereza hili, kuna wafungwa wa aina mbili: wafungwa wa kawaida na vilevile wafungwa waliotuhumiwa kwa uhaini.

Wafungwa wa kawaida ni wale wahalifu wanaopatikana na makosa mbalimbali katika jamii na kwa hivyo, wamefungwa kutumikia vifungo vyao na kuachiliwa huru baada ya kutamatisha vipindi vyao vya vifungo. Wafungwa kama hawa ni Polo na Hamadi Matope. Katika kiwango hiki, gereza linatekeleza jukumu la kuadhibu kwa njia ya kuwanyima wahalifu uhuru kwa kuwafungia – ambalo ni jukumu linaloafikiana na mawazo ya Foucault ya matumizi ya gereza kama chombo cha kuadhibu. Katika jamii anayoiandikia Shafi, gereza lina historia ndefu kama chombo cha kuadhibu. Analieleza kuwa kwa miaka mingi, limetumika kama maskani ya manunda waliofurutu ada ambao wameingiza na kutoka humo miaka nenda miaka rudi. Anaeleza kuwa, limemeza na kutema kila aina ya maasi, wahalifu waliobobea, waja wa laana waliotenda madhambi makubwa makubwa, wakasokomezwa humo kutubu madhambi yao.

Pamoja na kuwa gereza limetumiwa kwa miaka mingi katika jamii hiyo kuwaadhibu wahalifu, halijafanikiwa katika kurekebisha tabia na mienendo yao. Anavyosema Foucault, badala yake (kurekebisha tabia), gereza hukuza usugu miongoni mwa wahalifu. Katika *Haini* mwandishi ametoa kielelezo cha wafungwa wa aina hii kwa hivyo, kuthibitisha hoja hii. Mfano ni mahabusu anaowatumia Koplo Usi katika kupika na kuwagawia wafungwa wengine chakula. Mwandishi anawaeleza wafungwa hawa kuwa aghalabu ni wafungwa sugu, waliolelewa wakakulia mle gerezani, wakaizoea nyumba ile, wakaigeuza kuwa ndiyo maskani yao. Mwandishi anawaeleza kuwa machepe na mababe wanaolichukulia gereza lile kuwa mali yao na lililojengwa kwa ajili yao. Usugu wa wafungwa hawa unathibitisha namna ambavyo gereza halijafaulu katika kuwarekebisha wahalifu kitabia. Polo na Hamadi Matope ni mifano wa wafungwa waliotumia vipindi virefu cha maisha yao gerezani.

Kundi la pili la wafungwa ni washukiwa wa uhaini. Gereza limetumiwa kuwaadhibu wote waliotuhumiwa kwa uhaini. Hawa wamefungiwa sio kwa sababu ni wahalifu waliotekeleza mauaji ya Kigogo, bali kwa sababu watawala wanatumia nguvu na mamlaka yao kuwakandamiza. Wazo hili linalandana na mawazo ya Foucault anayesema kuwa, gereza hutumiwa kuunda jamii ya watu wanaochukuliwa kama wakosaji au wahalifu kwa kuwa wanadhaniwa kwenda kinyume na mfumo mzima wa mawazo au nguvu za watawala. Jamii kama hii ndiyo jamii ya mahaini inayoundwa katika *Haini*. Mwandishi akirejelea jamii hii anasema:

> *Lakini wa safari hii si maasi, si manunda, si waja wa laana, ni watu na heshima zao, watu na sharafa zao. Wengine mashekhe, wengine masharifu, wengine watu wenye uluwa*

> *wao, wake kwa waume, wamo humo, wamelemewa na jinamizi ndani ya gereza la Kinoamiguu.*
> *(uk 63).*

Ni dhahiri kwamba, jamii hii ya 'mahaini' ni jamii iliyoundwa na akina Kanali Bunju kwa manufaa yao wenyewe. Jambo hili linadhihirika kwa kuwa wengi wa washukiwa hawajui linalotendeka wanapokamatwa. Mfano ni Hamza ambaye anapokamatwa, hana habari kuhusu lililotendeka. Anapokea habari kuhusu kifo cha Kigogo akiwa gerezani. Tunasoma kuwa, "...*Hakuna aliyekuwa na matumaini kwani matumaini yote yalipeperushwa na shutuma za kutuhumiwa kwa kosa ambalo hakuna yeyote katika umati ule uliokata tamaa aliyelijua*" (uk 9). Nukuu hii ni thibitisho kwamba jamii ya 'mahaini' ni jamii iliyoundwa na wenye mamlaka katika jamii. Zaidi, ni dhahiri kwamba, jamii hii ya 'mahaini' haikuhusika katika mauaji ya Kigogo kwa kuwa tunaambiwa kwamba, mahaini wote waliotekeleza mauaji ya Kigogo waliuawa na Kanali Bunju.

Hali hii ya kuwafungia na kuwatenganisha 'wahalifu' imewaingia viongozi wengi akilini chambilecho Mandela (1990:188):

> *Katika mkabala huu serikali haitumii gereza kama asasi ya kurekebisha tabia, bali kama chombo cha kuadhibu; haitutayarishi kuwa watu wa heshima na maendeleo tufunguliwapo, bali kutuadhibu na kutulemaza ili tusiwe tena na nguvu ya kupigania maadili tuyathaminiyo.*
>
> (Tafsiri yetu).

Mambo wanayokumbana nayo akina Hamza na wenzake gerezani, yanafichua mengi tusiyoyajua katika moyo wa binadamu. Wanakabiliwa na mateso na dhuluma katika kiwango cha juu ili waweze kukiri kwamba, walihusika katika mauaji ya Kigogo.

### 3.1.2 Udhalimu na Ukatili

Udhalimu ni tendo la kufanya maovu na aghalabu huhusiana na matendo yasiyokuwa na huruma. Udhalimu uliopo katika jamii anayoizungumzia Adam Shafi unahusishwa na viongozi dhidi ya umma. Mfumo wa kigereza uliokita mizizi katika jamii hii, unatekeleza dhuluma kubwa za kukatisha tamaa. Watawala wanatumia mfumo huu katika kuwakandamiza raia kwa kuwashuku kuwa wahalifu.

Kwa mujibu wa nadharia ya Ki-Foucault, gereza kama mbinu ya kuadhibu ilianzishwa ili kuwaadhibu wafungwa kwa njia ya kuwanyima uhuru kwa kuwafungia ili ichukue nafasi ya kuwaadhibu wafungwa kwa njia ya kuwatesa. Lakini magereza ya kisasa yanatumia njia zote mbili; kuwafungia na kuwatesa wafungwa. Hii ndiyo moja ya sababu inayomfanya Foucault aseme kuwa, mifumo ya kisasa ya kuadhibu ni mibaya zaidi kuliko ilivyokuwa ile ya awali.

Katika *Haini* mbali na kuwa mahaini wanaadhibiwa kwa kufungiwa na kwa hivyo kutenganishwa na maisha huru, wanakabiliwa na mateso na dhuluma za hali ya juu ili waweze kukiri kwamba, walihusika katika mauaji ya Kigogo. Washukiwa wanadhulumiwa kimwili na kisaikolojia. Ukatili huu wanaotendewa wahalifu unatekelezwa kwa sababu ya nguvu rasmi walizonazo watawala. Mfumo wa kijamii hasa kwa kupitia sheria, unawapa

watawala nguvu za kuunyanyasa umma kwa ajili ya matakwa na faida yao. Mwandishi amesawiri jinsi wenye mamlaka wanavyotumia vitisho,hila, nguvu, uonevu na dhuluma kuwakandamiza watahumiwa wa uhaini.

Mwandishi amesawiri dhuluma dhidi ya washukiwa wa uhaini kutoka mwanzoni mwa riwaya ambapo tunaona watu wakishikwa ovyo ovyo kwa kutuhumiwa. Wanapelekwa katika kituo cha polisi ambako wanateswa na kupigwa kinyama. Kwa mfano, Hamza anapofikishwa katika Kituo cha Polisi cha Malindi anakaribishwa kwa kofi, pale anapomkuta rafiki yake, Barakati ambaye amepigwa sana, akatiwa pingu na kuvuliwa nguo zote, amepigwa sana kiasi kwamba amepoteza ufahamu wa kiswahili sasa anaongea kiingereza tu.

Gerezani washukiwa wanamosokomezwa, wanakandamizwa kwa dhuluma za aina mbalimbali. Tunawaona wanapofikishwa gerezani wote wanavuliwa nguo zao zote wakiwa pamoja, wanaume, wanawake na watoto. Hakika huu ni utovu wa heshima na utu. Viongozi wenye mamlaka wamesahau kwamba hawa ni watu lakini wanawachukulia kama vitu tu bali si binadamu walio na utu na heshima zao. Tunasoma:

> *"Vueni nguo! " aliamrisha mmoja wao... na pale alionyesha wazi wazi kuwa yeye ndiye mkubwa na mwenye sauti...Hamza akashangaa, akawatazama wenzake. Akafikiri, watavuaje nguo kwenye mkusanyiko kama ule! "Nasema vueni nguo!" sasa amri ilizidi ukali. Na naam nguo zilivuliwa. Wanaume uchi, wanawake utupu wa mnyama...wale waliokuwa wakiheshimiana, heshima iliishia pale na wale waliokuwa wakistahiana, staha iliishia pale.*
> *(uk 10)*

Adam Shafi ameonyesha namna viongozi wanavyotumia nguvu kuwakandamiza watawaliwa na kwa hivyo, kuwadhibiti. Hivi ndivyo nguvu inavyofanya kazi katika jamii kwa mujibu wa nadharia ya Foucault. Lengo kuu la viongozi katika kuwakandamiza raia ni kuwadhibiti. Enrich Fromm katika kitabu chake, *The Heart of Man* anaonyesha lengo la ukandamizaji. Amenukuliwa na Paulo Freire katika *Pedagogy of the Oppressed(1972)* akisema kuwa, ukandamizaji unahusisha kuwadhibiti wanaokandamizwa. Fromm anasema:

> *Raha iliyopo katika kumkandamiza mtu mwingine ni ukatili tu. Lengo la ukatili ni kumpotezea mtu utu na kumfanya kitu...kwa kuwa kudhibiti mtu kabisa kunampotezea uhuru wake wa kuishi.*
>
> (Tafsiri yetu).

Ni katika mkabala huu ambapo Freire anasema kuwa, sifa kuu ya wakandamizaji ni ukatili. Ili kumkandamiza, kumnyima uhuru na kumtawala, mkandamizaji huzuia njia zote za mkandamizwa kujikomboa. Hili ndilo tunaliona katika *Haini* ambapo raia hawana lingine ila kubaki wamedhibitiwa kwa kukandamizwa.

### 3.1.2.1 Mazingira Dhalilishi

Mazingira ya vyumba wanamowekwa wafungwa, yanaendeleza picha ya dhuluma dhidi yao. Mfungwa hufungiwa katika chumba akiwa peke yake au katika chumba akiwa pamoja na wengine. Mshukiwa anapofungiwa katika chumba peke yake kunamdhulumu kisaikolojia kwa kuwa hali hii, inamtenga na binadamu wengine na kumwacha kusononeka kwa upweke. Kwa mfano, Hamza anafungiwa peke yake katika chumba cha kiza. Kuna vyumba ambamo wafungwa waliwekwa kwa makundi, kwa mfano chumba cha akina

Hamza, Sururu, Shekhe Mandundu, Shadidi, Kombo, Abdul, Fimbo, Bilali na Nassor kule Kumbakumba.

Mwandishi ametuchorea taswira ya vyumba wanamofungiwa wafungwa na kutuonyesha namna hali yao ilivyodhalilishwa na kudunishwa. Anatueleza kuwa, vilikuwa vyumba vitupu, havikuwa na chochote cha kulalia. Mle ndani mlikuwa na mtondoo tu, ambao ulikuwa ndicho choo chao. Je, itakuwaje mtu kukaa chumba kimoja na kinyesi chake? Chumba chenyewe kimezibwa kila mahali! Usiku huminimika mbu vyumbani. Mle ndani mmejaa wadudu wa aina zote wapendao mazingira ya uchafu.

Mazingira ya chumba cha kiza yanadhulumu hata zaidi kuliko vyumba vingine mle Kumbakumba na kwa Ba Mkwe. Baada ya Hamza kukataa ushawishi wa Kanali Bunju na wenzake wa kumtaka akiri kuhusika katika uhaini ili awe shahidi wao mahakamani, Bunju anaagiza Hamza apelekwe katika chumba cha kiza. Chumba hiki anavyokisawiri mwandishi ni chumba cha kudhalilisha sana.Tunasoma:

> *Kiko katikati baina ya Kumbakumba, chumba cha kunyongea na jiko. Mlango wake ni wa chuma na jua la mchana kutwa hupiga mlangoni hapo. Ukuta wa chumba hicho umeshikana na jiko na kuni zote zinazoteketea jikoni hapo humimina joto lake ndani ya chumba hicho. Mchanganyiko wa joto la moto wa jikoni na joto la jua linalopiga juu ya ule mlango wa chuma mchana kutwa ndio unaotengeneza hali ya hewa ya chumba cha kiza. Joto kali hufukuta chumbani humo kutwa, kucha na inapofika usiku, mbu humiminika humo utadhani wanamiminiwa makusudi (uk 85).*

Hii ndiyo iliyokuwa hali katika chumba cha kiza. Ilimwia Hamza vigumu kusimama, kuketi au hata kulala mbali na kuwa katika hali ya upweke na njaa. Anatolewa mle chumbani baada ya siku kumi na mbili huku amezidiwa na homa kali.

Dhuluma dhidi ya washukiwa hazikuisha tu na vyumba vya kumbakumba, kwa Ba Mkwe na Chumba cha Kiza. Kuna Mashakani Hotel. *"Huku ndiko wanakopelekwa watu wakafichwa kwa miaka kadhaa wasijulikane walipo na hatimaye wakatokomea kabisa"* (uk 168). Ni jumba ambalo limefichika katikati ya chaka kubwa. Haramia anapotaka kuwashawishi wenzake wasikubali kuwa mashahidi katika kesi ya uhaini dhidi ya wenzao, huku ndiko anakopelekwa baada ya kusalitiwa na Pwacha. Haramia anafungiwa chumba kimoja na chatu ili yule chatu amle atakapohisi njaa. Ujasiri na mauti yanayomkabili Haramia unamfanya kumenyana na yule chatu na Haramia anafaulu kumwua kwa kumkata shingo kwa meno yake.

Mazingira ya vyumba yanayokandamiza ni jambo linalodhihirika katika kazi nyingi za fasihi ya kifungoni kwa mfano, Kihoro katika *Never Say Die* (1998) anaeleza kwamba, wakati mwingine mfungwa alitiwa ndani ya chumba kilichokuwa na maji tele na kuachwa kupoozea mle kwa siku kadhaa. Naye Jackson (1971:8) anaeleza hali ya vyumba vya gereza walimofungiwa wafungwa wenye asili ya Kiafrika kule Marekani. Anasema kuwa, mfungwa alifungiwa katika chumba chenye kiza ambacho sakafu na kuta zake zilizochakaa zilifunikwa kwa kinyesi cha wafungwa waliokuwamo. Siku saba aliachwa uchi na hakuruhusiwa kuoga. Hakukuwa na chochote mle ndani isipokuwa shimo la choo katika sakafu.

Katika *Haini,* watuhumiwa pia wamenyimwa fursa ya kutekeleza usafi wa mwili. Kuoga na kunyoa nywele ni mambo ambayo yalikuwa nadra mle gerezani. Pamoja na hayo, mavazi yao ni matambara. Mwandishi anapotoa taswira za wafungwa hawa anasema kuwa, ule wasifu wa sura zao za kibinadamu umeanza kupotea, wamekuwa kama hayawani, manywele machafu yamewasimama timutimu, yamesokotana, yameshiba vumbi na kuzongwa na nyusi za magunia. Anaendelea kueleza kuwa, nyuso zao zimesongwa na madevu yaliyoota ovyo ovyo yameshikana na misharabu iliyotambaa juu ya midomo yao ikatoa miche mithili ya magugu na kuifunika midomo yao. Kinyatti (1996) akigusia tajriba zake gerezani anasema kwamba, wafungwa wengi huvaa matambara yaliyovamiwa na chawa ambayo hunuka kinyesi, si ajabu kuwaona wafungwa wakitembea uchi.

### 3.1.2.2 Uhaba Wa Chakula

Chakula hutumiwa kama mbinu ya kuendeleza dhuluma. Gerezani chakula ni haba pamoja na kuwa hakipikwi vizuri. Watuhumiwa wanateswa kwa kunyimwa chakula kizuri na cha kutosha. Kile kidogo wanachopewa kinachochea njaa badala ya kukidhi haja. Mwandishi anasema kuwa, asubuhi waligawiwa kikopo cha uji na kipande cha muhogo. Mchana, muhogo wa kuponda na majani yake, wakakipa chakula hicho jina la *"full suit"*. "*Mazungumzo yao yote mle chumbani yakawa juu ya mlo, kula na mipishi. Wakazungumza kula, wakaota kula, wakapika kwa mawazo, lakini wapi, njaa ikawatawala mle gerezani mtindo mmoja".* (uk 22). Katika chumba cha kiza Hamza anapewa chakula kidogo sana. Rafikiye, Hamadi Matope ambaye ni mfungwa mpishi, anamfaa kwa kumlisha rojo ya maharagwe iliyochanganywa na wali akitumia mpira wa kumwagia maji bustanini.

Viongozi wanatumia mbinu ya uhaba wa chakula kuwakandamiza washukiwa ili wakiri kwamba, walishiriki katika uhaini. Hamza anaposhawishiwa na Kanali Bunju akiri kushiriki, anaahidiwa kuwekwa mahali pazuri. Mahali wale wengine tisa waliokiri wamewekwa wanapopewa pilau, chai ya maziwa, mikate, siagi na "jam". Akiwarejelea wale tisa, mwandishi anasema:

> *Chumba chao sio cha wale wanaolishwa muhogo na majani yake asubuhi na jioni. Hapa vinaliwa vyakula vinono vilivyoandaliwa kwa ajili yao tu ikiwa ni jaza yao ya kwenda kukubali kukiri kosa na kwenda mahakamani kutoa ushahidi dhidi ya wengine.*
> *(uk 154)*

### 3.1.2.3 Kunyimwa Huduma za Matibabu

Gerezani walimo watuhumiwa hamna huduma za matibabu. Wanakandamizwa kama kwamba wao si binadamu wanaostahili kupata huduma bora au huduma zozote za matibabu. Wanapoteswa, yale majereha yanapona kwa hisani ya mwenyezi Mungu kwa vile hawapati huduma zozote za matibabu. Kwa mfano, Sururu anapotiwa katika chumba cha akina Hamza ameumizwa sana, mwili wake umevunda, unakenyakenya na unatoja rojo ya usaha. Mgongoni mmefanya mashata ya damu na usaha juu ya misirimbo ya michapo mikali ya fimbo na viboko iliyomzonga mdawari mgongoni kuzungukia mbavuni mpaka tumboni. Akina Hamza wanamsafisha yale madonda yaliyomjaa mwili mzima, huku akiugua na kusononeka kwa ukali wa maumivu anayopata.Tunasoma: "*Chumba kizima walikuwa wauguzi na Abdul ndiye muuguzi mkuu wa kuyatumbua-tumbua yale mashata ya usaha na kumsafisha*" (uk 21).

Kule kwa Ba Mkwe, Hamza na Doto wanaugua na kuuguzana bila ya msaada wa matibabu maalum. Vilevile, Hamza anapougua mle chumba cha kiza, hashughulikiwi kwa vyovyote. Anapomwarifu Koplo Usi, hana haja na ugonjwa wa Hamza. Anapokea matibabu anaporejeshwa kwa Ba Mkwe baada ya kuzidiwa na homa.

Aidha, mmoja wa watuhumiwa anakosa kufika mahakamani kwa kuwa amefariki kwa kuugua tumbo la kuhara. Kwa mujibu wa wafungwa wenzake, Amhasi Ahmed anafariki kwa kukosa matibabu.

### 3.1.2.4 Kupigwa kinyama

Matumizi ya nguvu kwa kuwadhulumu wafungwa yanafikia kilele kwa kipigo cha kinyama. Mateso haya yanaweza kulinganishwa na mateso ya hadharani yaliyotekelezwa kwa wahalifu katika 'Enzi ya Mateso' kule Ulaya kabla ya kuanzishwa kwa gereza kama njia ya kuadhibu. Inaonekana hii ndiyo moja ya mbinu kuu za kuwatesa wafungwa zinazotumiwa na wenye mamlaka kwa kuwa ni masimulizi ambayo yameenea pakubwa katika kazi za fasihi ya kifungoni. Ngugi (1991), Kihoro (1998) na Kinyatti. (1996) pia wamelizungumzia jambo hili.

Kule kwa Ba Mkwe Hamza na wenzake wanapigwa kinyama ili wakiri kuwa walihusika katika uhaini. Wanatwangwa kwa fimbo za mipera mpaka wengine wanapoteza fahamu na wengine kufariki. Udhalimu huu unatekelezwa na wanajeshi waliokuwa na vyeo vya juu, wenye mamlaka, nguvu na uwezo.Tunasoma: *"Wale wanajeshi walikuwa ni wa vyeo vya*

*juu waliobeba tepe nzito mabegani. Kila moja wao alikuwa na gongo la mpera mkononi. Magongo yenyewe yamekaa kama mapikipiki ya kupopelea embe"* (uk 37-38).

Taswira ya mateso ya Hamza anayoisawiri mwandishi kule kwa Ba mkwe, ni kielelezo cha namna walivyoteswa washukiwa kwa kutwangwa sana. Tunaambiwa kuwa, askari wa usalama alimtwanga Hamza kwa gongo la mpera kichwani, damu ikamwagika na kutapakaa kote; juu ya makaratasi, nyingine chini na nyingine ikachuruzika usoni. Wengine wote wakamwingilia kama nyuki aliyechokozwa. Alipigwa mpaka akashindwa kusimama kwani hawakuchagua pa kupiga. Mle ofisini:

> *Alivishwa kitanzi shingoni wakamburura huku na huku na yeye akawafuata kama ng'ombe aliyevishwa shemere. Damu ikimwagika, denda likimchururika. Alipiga kelele kuomba huruma yao mpaka sauti ikapotea ikawa haitoki tena. Lakini huruma itoke wapi nyumba ile. Alibaki kukoroma tu.*
> *( uk 40-41).*

Kuna wengine waliopigwa hadi wakafa na hakuna lolote walilotendewa wale madhalimu. Chumbani anamofungiwa Hamza anaikuta maiti ya Kidau ambaye amepigwa hadi akafa. Maiti inachukuliwa usiku kwa kutiwa ndani ya gunia. Udhalimu wa aina hii ni sawa na ule uliofanyiwa wafungwa wa kisiasa kule Afrika Kusini wakati wa Enzi ya utawala wa ubaguzi wa rangi. Kwa mujibu wa Buntman (2003:18), washukiwa walifungwa bila kuhukumiwa na mle gerezani wakati mwingine waliteswa hadi wakafa.

Mwandishi pia amesawiri namna Doto anavyoteswa. Yeye ni mwanajeshi mwenye ushujaa mwingi, anajaribu kubishana na kupambana na wale madhalimu lakini yote yanakuwa ni

kupiga ngumi ukuta. Anaumizwa sana, hasa makorodani yake. Anatiwa ulema na hata baadaye, anapotembea huichanua miguu yake kama aliyetiwa jandoni kutokana na maumivu marefu ya makorodani.

Watuhumiwa pia, huchukuliwa usiku kutoka vyumbani mwao na kupelekwa mahali ambapo wanateswa. Hamza anachukuliwa usiku kutoka chumbani alimowekwa yeye na Doto. Anapelekwa mahali anapopigwa, kusomekwa tambara kinywani linalomjaa, kuzongwa kamba mwili mzima inayomkaza sawasawa na kulaaniwa na kutukanwa. Halafu ananing'niziwa ndani ya kisima, kichwa chini na miguu juu , akiwa anafyatuliwa risasi zinazomkosa chupuchupu. Tunaelezwa kwamba, hewa ya mle kisimani imejaa ukungu naye anatoswa majini, uhai wake unahifadhiwa tu na ujuzi wake wa kupiga mbizi.

Kuna mifano mingi riwayani inayoonyesha namna viongozi wanavyotumia nguvu kuwakandamiza washukiwa kwa njia ya kuwatesa. Tulivyosema kwingine, lengo lao ni kuwashurutisha wakiri kuhusika katika uhaini. Wale wanaoshindwa kustahimili mateso haya, wanakiri. Wanakiri sio kwa sababu walihusika lakini kwa kutaka kuponya roho zao.

Kwa mfano, tunamwona Marzuku, mmoja wa washukiwa wale tisa akiwaza na kujuta kwa kubuni kisa, akakiremba na kuwajaza mahaini wote, kila mmoja na jukumu lake. Lakini alitenda lile kwa sababu ya kuteswa. Tunasoma:

> *Lakini angefanya nini siku ile waliyomvamia, wakamtwanga, wakamfundafunda, wakamninginiza kwenye kitanzi mavi mabichi yakamtoka, "Ningefanya nini na wao wamenisimamia kama Ziraili wanaitaka roho yangu?"*

*(uk 153).*

### 3.1.2.5 Mateso ya Kisaikolojia

Kisaikolojia, washukiwa wanateswa kwa njia mbalimbali. Wanafungiwa katika mazingira ya upweke hali ambayo inawasababishia kusononeka. Mfano wa Hamza anayefungiwa katika chumba cha kiza na Haramia anayefungiwa chumba kimoja na Chatu. Kufungiwa gerezani pia kunawatenga na familia zao kule nje. Sheria za nchi hii ni kama haziruhusu wafungwa kutembelewa na jamaa zao au kama zinaruhusu, basi sheria hiyo haitekelezwi.

Katika *Haini* tunawaona wafungwa wakiwaza na kusononeka sana kwa sababu ya mawazo ya familia zao kule nje. Nassor na Hamza ni mifano wa wafungwa ambao tunakumbana nao wakiwa ndani ya mawazo mengi wakati mwingi. Kule Kumbakumba Nassor anamlilia mkewe na watoto wake hadi wakampa jina la *"Big Baby"*. Hamza naye wakati mwingine, tunamwona akimuwaza Khadija na mtoto wake.Tunasoma:

> *Mawazo yale yalimjaa kichwani mpaka kichwani humo mkawa hamna nafasi ya kuwaza jengine lolote zaidi ya Khadija, mke wake mpenzi. Ametenganishwa naye kwa kuwekewa senyenge, akaekewa na askari wa kumlinda na bunduki mkononi, na walinzi wengi waliokaa makini.*
> *(uk70).*

Kinyatti (1996) na Sithole (1976) wana tajriba kama hizi katika maisha yao gerezani. Katika jamii zao, kutembelewa gerezani ni jambo lililowekewa vikwazo vingi, na iwapo mtu alitembelewa mgeni alipewa dakika chache za kuonana naye kupitia kwa waya au

kioo. Hali hii ya wafungwa kutenganishwa na familia zao inawazulia mahangaiko na mateso ya kiakili.

### 3.2 Adhabu za Kigereza Katika Jamii Pana

Kwa mujibu wa nadharia ya Ki-Foucault, mfumo wa kuadhibu wa Kigereza umeenea katika jamii nzima kwa kile anachokiita 'Bahari ya Kigereza' au 'Mji wa Kigereza'. Foucault anasema hivi kwa kuwa mfumo wa kisasa wa kuadhibu, unadhibiti maisha ya kila mtu lifanyavyo gereza. Gereza limesawiriwa kuwa sitiari ya jamii zetu na kwa kutumia taswira hii, mwandishi wa *Haini* anadokeza mfanano uliopo baina ya gereza na maisha yaliyo nje ya gereza.

Mbali na kuwa matukio mengi ya riwaya hii yamejengwa katika mazingira na tajriba za gerezani, mwandishi ameyamulika maisha yaliyo nje ya gereza na kuonyesha namna yalivyo na mfanano na yale ya gerezani kwa kiwango fulani. Dhuluma sio tu zinawakumba wafungwa gerezani, bali pia watu huru kule nje ya gereza. Kwa kiwango kikubwa mwandishi ametumia mateso ya familia ya Hamza kule nje, kuwa kielelezo cha familia za mahaini.

Ukosefu wa chakula si taabu inayolikumba gereza pekee, bali sifa ya jamii nzima. Tunapoitazama familia ya Hamza kule nje, tunaona wanavyoishi kwa taabu ya kuvipata vyakula; kupata bidhaa kama vile mkate na mchele ni tatizo kubwa. Tumeonyeshwa Khadija akihangaika anapotaka mkate. Khadija anasema kuwa, ukienda kwenye duka la ukoo kama siku yako haikufika, hata ukilia machozi ya damu mchele haupati. Mkate

kupatikana ni vigumu. Watu hupanga foleni ya mkate tokea usiku na hukesha hapo kusubiri mkate wa asubuhi. Hata hivyo, mkate huo wenyewe hupatikana kwa bahati nasibu tu. Katika duka la Awidhi hakupatikani bidhaa. Mzee Maftah anapotafuta kiambatanishi cha kunywea chai, hapati chochote huko.

Kuna ukosefu wa chakula katika nchi nzima. Masanja anakamatwa kwa sababu ya kununua unga wa Magendo kule Kombeni. Abdul naye akiwa gerezani, anaeleza kuwa nchini kuna ukosefu wa sukari na mchele lakini ukiongea unatiwa ndani.

Khadija vilevile anakabiliwa na dhuluma za kila aina kule nje. Tumeambiwa kwamba amefukuzwa nyumbani kwake kwa kushindwa kuilipia nyumba, tukio linalomfanya kuhamia Kisimamajongoo kwa wazazi wake. Azizi, mmoja wa maafisa wakuu serikalini anatumia fursa ya hali inayomkumba Khadija kumkandamiza kimapenzi. Kwa ujumla, wake wa mahaini wanaonwa kama mahaini na wamekuwa watu wa kutorokwa, kwa hivyo wanakaa kwa pweke walivyo wafungwa gerezani. Kwa mfano Baraka, na mkewe wanamtoroka Khadija kwa kutotaka kuhusishwa na mahaini.

Kisaikolojia, jamaa wa familia za Mahaini wamekolezwa mateso kwa kutenganishwa na jamaa wao. Familia nyingi zimesambaratika kwa kuwa watu wengi wamekamatwa na kufungiwa gerezani. Tunaona vile Khadija anaumia kimawazo kwa fikra za mumewe ambaye haijui hali yake wala hatima yake. Ni dhahiri Khadija ameumia kiasi kwamba, amethubutu kutafuta njia za kumwokoa Hamza kutoka katika janga lilomfika; anajaribu kwa Baraka – anamtoroka, anafikiria Azizi atamponya – anakuwa mnafiki mkubwa, naye

mganga, Kidongo Chekundu, hakumfaa. Hatima yake ni mawazo, mchana kutwa na usiku kucha kumhusu Hamza.

Naye mkewe Khalfani, maisha yamemwia magumu kule nje. Mwanamke huyu amekata tamaa na kudai talaka kwa Shekhe, sasa ameolewa na mume mwingine. Khalfani mle gerezani amepata ujumbe huu, anaumia ndani kwa ndani. Kila siku anakonda.

Hali ya maisha ya familia za wafungwa, kama inavyosawiriwa katika kazi nyingi za fasihi ya kifungoni, zinaishi maisha ya Kigereza wanavyoishi jamaa wao walio gerezani. Katika ujumbe wake kwa Maina wa Kinyatti akiwa gerezani, Jeff Mwangi anamwambia: "Kumbuka sio wewe pekee uliye gerezani, sisi sote tumo gerezani kwa kuwa tunaishi katika taifa linalotawaliwa na askari" Naye Mumbi, mkewe, anamwambia, "...mambo si mazuri huku nje. Ukatili umezidishwa. Watu wengi sana wamekamatwa, wengine wanateswa kule Nyayo House na wengine wengi wamepotea"(Kinyatti, 1996:186). Nukuu hizi ni mfano wa kuthibitisha namna jamii zetu zilivyo za kigereza kimwelekeo.

## 3.3 Nguvu na Matumizi Mabaya ya Mamlaka

Nguvu rasmi katika jamii anayoizungumzia Shafi, zimo mikononi mwa wanajeshi na viongozi wakuu serikalini. Wanajeshi wenye mamlaka ni kama vile Kanali Bunju. Nao viongozi wakuu serikalini wenye mamlaka ni kama vile Mheshimiwa Kigogo, ambaye ameuawa, na Chopra, mwendesha mashtaka wa serikali. Hawa ni vielelezo tu vya watu wenye vyeo na mamlaka, jeshini na serikalini, wanaoendesha shughuli za utawala za kila siku katika jamii hii. Hali anayoisawiri Shafi kuhusu nguvu katika riwaya hii, inaiafiki hali

anayoieleza Pradhan katika, "Politics of Power Structures" katika, Trivedi. (1984:186). Pradhan amemnukuu Mills (1956). katika kitabu chake, *The Power Elite,* ambaye anasema kwamba:

> *Nguvu rasmi, hazipo tena mikononi mwa matajiri kama ilivyokuwa hali ya awali. Nguvu rasmi, ambazo zinamaanisha nguvu za kisiasa, sasa zipo mikononi mwa wanajeshi na watawala serikalini. Watu hawa wanadhibiti miundo ya nguvu na wanajali maslahi ya kuwanufaisha wenyewe.*
>
> (Tafsiri yetu)

Kuwaadhibu watu kwa kuwafungia na kuwatesa bila haki, namna ilivyo katika *Haini* ni zao la moja kwa moja la matumizi mabaya ya mamlaka. Riwaya ya *Haini* imesawiri namna viongozi wanavyotumia mamlaka waliyopewa kuwanyanyasa na kuwakandamiza raia. Viongozi wanatumia sheria, vyombo vya dola kama vile gereza, askari na mahakama kuwakandamiza raia. Hali ilivyo katika *Haini* inaafikiana na Nadharia ya Ki-Foucault inayodai kuwa, katika jamii za Kigereza viongozi hutumia nguvu walizopewa kuwanyanyasa watawaliwa. Nguvu za viongozi hutokana na mfumo wa kisheria ambao Foucault anasema umeundwa kuwanufaisha wachache wenye nguvu na kuwakandamiza wengi. Oruka (1976:3) anasema kuwa, viongozi sio sheria bali vyombo vya kutekeleza sheria. Wakati mshukiwa wa uhalifu au mhalifu anapoadhibiwa, ni sheria inayomwadhibu. Anaendelea kusema kuwa, wakati sheria inapowapa watu mamlaka ya kuwaadhibu wahalifu au washukiwa wa uhalifu, watu wale hutumia sheria kwa manufaa yao wenyewe. <u>Kwa hivyo, hawatekelezi matakwa ya sheria ila matakwa yao kwa kuivunja sheria</u> (msisitizo wetu). Hili ndilo linalotokea katika *Haini.*

Mazungumzo ya wafungwa, Hamza, Faraji, Ambar na wengine yanaonyesha namna mfumo wa kisheria unavyotumiwa kuwanyanyasa. "*Kutuweka ndani muda huu wote, kututesa walikotutesa, wewe unafikiri kuna sheria hapa?*" aliuliza Ambar. Faraji naye anasema, sheria ipo, tatizo ni kuifuata au kutoifuata. "*Kumtesa mtu halafu ukamlazimisha aseme uongo ndo kufuata sheria huko?*" aliuliza Khalfani (uk 136).

Nguvu katika jamii hii inatokana na mifumo mbalimbali katika mazingira anayoyasawiri Shafi. Mifumo hii hasa ni ya kisiasa na ya kijamii. Mifumo hii imewapa watu kama akina Kanali Bunju nguvu na mamlaka juu ya wengine. Mifumo hii imeigawa jamii Kitabaka ambapo tabaka la juu linatumia nguvu na mamlaka kulinyanyasa na kulikandamiza tabaka la chini. Tabaka la chini ni la raia wa kawaida na watu wote ambao hawakuafikiana kimawazo na Kanali Bunju. Hili ni kundi dhaifu lisilo na sauti.

Uongozi ulio katika jamii ya mwandishi umewasawiriwa kuwa uongozi wa kiimla. Uongozi unaojali maslahi ya tabaka la viongozi huku watu wengi wakiumia. Uongozi huu umekuwa chanzo cha matatizo yanayoukabili umma. Mosi, Mheshimiwa Kigogo ambaye ni kiongozi wa nchi, anakandamiza asasi za sheria katika taifa hili. Siku za uongozi wake, Kigogo alizivunja mahakama za mahakimu na akaziunda mahakama zake alizoziita "Mahakama za Wananchi." Hivi ndivyo wahusika waliobobea katika sheria kama vile Faraji wanavyojikuta wakiwa raia hohehahe. Kinaya ni kwamba, Pandu, mwuza samaki; Jongo, mwuza maziwa; na Musadiq, mwalimu wa chuoni ndio mahakimu katika mahakama kuu. Vilevile, Kigogo anatumia mamlaka yake kuvivunjilia mbali vyama vya

wafanyakazi. Hali hii inaonyesha kwamba wanaopewa mamlaka ya kuwaongoza wengine huyatumia mamlaka yao vibaya.

Viongozi wanatumia vyombo vya dola kama vile gereza, polisi na mahakama katika kuudhibiti umma. Matumizi mabaya ya vyombo hivi yanadhihirisha namna viongozi wanavyotumia mamlaka vibaya. Wasimamizi wa gereza la Kinoamiguu, askari pamoja na wanajeshi wamesawiriwa kama watu waliojaa unyama usiomithilika kutokana na mateso wanayodhihirisha dhidi ya washukiwa wa uhaini. Viongozi mahakamani kama vile Chopra, mwendesha mashtaka wa Serikali, anatumia cheo na nguvu katika kuwakandamiza washukiwa wa uhaini. Kwa hila na maonevu, anawasilisha kwa ustadi mashtaka ya uwongo dhidi ya mahaini.

Mfano wa jamii anayoisawiri Shafi katika *Haini* ni jamii inayosawiriwa na Orwell katika *Shamba la Wanyama* (1967), ambapo sheria zinatumiwa kwa maslahi ya wachache tu na mateso ya wanajamii yanafikia kiwango cha juu sana. Jamii za aina hii ni za Kigereza ambamo watu wanadhibitiwa na kwa kiasi fulani, kuundwa na miundo ghibu ya nguvu rasmi. Mifano mingine katika fasihi ya Kiswahili ambapo hali hii inadhihirika waziwazi ni katika riwaya mbili za Mkangi: *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995). Riwaya hizi sawa na *Haini,* zinaonyesha jinsi mfumo uliopo katika jamii zenye dhuluma unavyoundwa ili kuhakikisha wanyonge wanadhibitiwa na kutawaliwa kwa kila njia. Zinaonyesha jinsi jamii zinavyogeuzwa za kigereza na jinsi uhuru wa wengi unavyodhibitiwa na tabaka la viongozi wachache.

## 3.4 Uchungulizi

Kwa mujibu wa Foucault, moja katika sifa kuu za jamii ya kigereza ni uchungulizi. Hii ni jamii ambayo daima inachungulia na kuchunguliwa. Wazo hili linaenda sambamba na dhana ya mnara wa uchungulizi wa gereza wa Jeremy Bentham, dhana ambayo imeiathiri jamii nzima.

Gereza la Kinoamiguu limejengwa kwa muundo uliopendekezwa na Bentham ambao Foucault anauzungumzia . Pana mnara wa uchungulizi ambapo pana askari anayewalinda wafungwa wakati wote. Kwa mfano, Sururu anapojaribu kutoroka kutoka gerezani, Koplo Ngwali aliye mnarani anamwona huku Sururu akiwa hafahamu. Katika milango ya vyumba vya wahalifu pametobolewa tundu ambazo walio ndani wanaonekana lakini walio ndani hawawaoni wa nje. Huu ndio muundo wa jela imara aliyopendekeza Bentham. Mbali na kuwa wamefungiwa, askari hawabanduki na bunduki kuwalinda kila mara na wakati. Muundo huu wa gereza kama lilivyo gereza la Kinoamiguu, unawafungia na kuwadhibiti wafungwa kimwili na kimawazo.

Jambo analolitilia mkazo Foucault kuhusu muundo huu wa Kigereza, ni namna ulivyoiathiri jamii pana. Gereza limesawiriwa kuwa sitiari ya jamii pana. Mnara huu wa uchungulizi ni sitiari ya serikali ambayo ina uwezo wa kuyachungulia maisha ya raia. Viongozi wanatumia mbinu mbalimbali katika kuchungulia mienendo ya raia. Wale raia walio na mawazo yanayokinzana na ya viongozi, hukamatwa na kutiwa gerezani. Moja katika mbinu za uchungulizi zinazotumiwa katika *Haini* ni ujasusi. Viongozi wana watu

maalum wanaodadisi na kufahamu kinachosemwa na watu. Kwa mfano, Zonga amewekwa gerezani miongoni mwa mahaini ili awachunguze.

Kuna mifano zaidi ya wahusika wanaotumiwa na viongozi wakuu Serikalini kudadisi wanavyosema watu. Haramia ni mmoja wao, kabla ya mauaji ya Kigogo. Anavyosema mwandishi, Haramia alikuwa ni mmoja wa vitimbakwiri vya Kanali Bunju alivyovisambaza kila pembe vikinusa na kuduhushi mambo na kumpelekea habari. Naye Faraji ameajiriwa na Kapera, afisa mkubwa katika Idara ya Usalama. Kazi yake ni kumtafutia habari. Nani anasema nini, huyu anafanya nini, yule anaongea nini.

Baada ya Kifo cha Kigogo, hali hii imeendelezwa zaidi. Hali ambayo imesababisha hofu miongoni mwa wananchi. Watu wanazungumza kwa minong'ono kwa kuwa, hakuna anayemwamini mwenzake. Tunamwona Bi. Farashuu akimwonya Khadija azungumze kwa sauti ya chini asije akasikika likawazukia balaa anaposema kuwa siku hizi kila pahali pana foleni, anapotaka kwenda kununua mkate.

Katika hali, hii mwandishi anaeleza kwamba mji umepwaya kimya, utadhani umeelemewa na jinamizi, nyoyo za watu zimejaa hofu na wasiwasi. Hakuna anayejua lini au saa ngapi atatiwa mbaroni, watu wanakwenda na kurudi kila mmoja akiwaza labda sasa hivi au halafu. Mwandishi ameendelea kueleza kwamba, waliokuwa wakizungumza, wakinong'ona, kwa kuwa roho za watu zimekosa imani na hakuna anayemwamini mwenzake. Kila mmoja anamwona mwenzake kuwa jasusi.

Kwa mujibu wa Foucault, lengo kuu la matumizi ya mfumo wa Kigereza katika jamii pana, ni kuudhibiti umma kwa kuzalisha jamii tiifu. Hili ndilo tunaloliona katika *Haini* ambapo tunaiona jamii iliyodhibitiwa kabisa na serikali; watu wanaishi kwa hofu kuu na kutenda mambo kulingana na matakwa ya serikali bila kulalamika kwa njia yoyote ingawa wanateseka sana. Kwa Foucault, hiki ndicho kilele cha kuudhibiti umma kwa kuwa watu sasa, wanajilinda wenyewe kwa hofu kwamba matendo yao yataonekana hata kama wayatendayo hayaonekani.

## 3.5 Hitimisho

Sura hii imeangazia jinsi mwandishi Adam Shafi ametumia taswira ya gereza kuendeleza maudhui katika riwaya yake ya *Haini.* Imebainika kwamba, asasi ya gereza haitumiwi katika kuwarekebisha watu tabia, bali inatumiwa kama chombo cha kuunda jamii ya wahalifu na kwa njia hiyo, kuidhibiti jamii hii kwa kuitesa na kuidhalilisha. Ni asasi inayotumiwa na wachache wenye mamlaka kutekeleza matakwa yao. Athari za gereza hazionekani tu katika gereza, bali pia zinavuka mipaka na kuwaathiri walio nje ya kuta za gereza. Mwandishi ameonyesha ufanano uliopo kati ya gereza na maisha yaliyo nje ya gereza. Sura hii vilevile imeonyesha namna masuala ya adhabu na nguvu yanavyosawiriwa na kuendelezwa katika *Haini.*

# SURA YA NNE

# ATHARI ZA JAMII YA KIGEREZA KATIKA *HAINI*

## 4.0 Utangulizi

Katika sura ya tatu tumechunguza namna sifa kuu za jamii ya kigereza kwa mujibu wa nadharia ya Ki-Foucault zinavyojitokeza katika riwaya ya *Haini.* Tumeona namna suala **la kuadhibu, nguvu (mamlaka), na uchungulizi** yanavyosawiriwa katika *Haini.* Kwa maoni yetu jamii anayoisawiri Adam Shafi ni jamii ya kigereza kimwelekeo. Tumegundua kwamba wakati miundo na mifumo ya jamii inapofanya kazi kigereza, hali hii ina athari kubwa katika jamii. Kuna namna ambavyo maisha ya watu yanavyoathiriwa na hali hii, na hili huwa ni zao la moja kwa moja la mifumo ya **nguvu** inayofanya kazi katika jamii ili kuudhibiti umma. Katika sura, hii tunalenga kujadili athari hizi kama zinavyojitokeza katika *Haini.* Kwa ujumla, jamii ya kigereza inayosawiriwa katika *Haini* ni jamii inayokumbwa na usaliti, ubinafsi, kutoaminiana, hofu, ubarakala, ukosefu wa haki na ni jamii iliyokata tamaa kwa kuwa watu wamedhibitiwa kabisa kiasi kwamba hawana namna ya kujikomboa.

## 4.1 Usaliti na Ubinafsi

Riwaya ya *Haini* imejaa visa vingi vya usaliti. Baadhi ya wahusika wametenda vitendo vingi ambavyo vimeitumbukiza nchi yao katika mashaka na misukosuko. Vitendo hivi vyote vinatekelezwa kwa sababu ya maslahi ya kibinafsi.

Katika riwaya hii, usaliti unajitokeza kwa njia mbalimbali. Mosi, Kigogo ambaye amefanikiwa kuwaongoza wakwezi na wakulima katika kuuondolea mbali utawala wa kisultani anasalitiwa na viongozi wenzake, walio karibu naye – ambao kwa hakika ndio wanapanga njama ya kuipindua serikali yake. Njama hii inasababisha kifo cha Kigogo. Jambo hili la kusalitiwa na viongozi wenzake linathibitishwa na Haramia ambaye tunamwona akimwambia Kuchi: "*Sikiliza Kuchi. Haya mambo kuna wenyewe wanayoyajua. Wanayajua utando mpaka ukoko. Kuna wenyewe waliyapanga...wakubwa! wakubwa wenyewe ndio waliyapanga haya"* (uk. 158). Haramia haelewi ni kwa vipi silaha zingeweza kuibwa kutoka ghala la kuzitunzia wiki nzima kabla ya mauaji ya Kigogo, wakubwa wakijua hayo na kutochukua hatua yoyote. Mauaji ya Kigogo ndio usaliti unaokitumbukiza kisiwa cha Zanzibar katika mashaka na misukosuko, hali ambayo inaiingiza jamii hii katika maisha ya Kigereza.

Wananchi wa kawaida; wakulima na wakwezi walitumia mapanga na mashoka kuangusha uongozi wa Sultani. Matumaini yao ya kuwa na maisha bora, yanadidimia kwani serikali ya Kigogo waliyoiweka mamlakani iligeuka ya kuwakandamiza. Baadhi ya mambo anayoyatenda Kigogo ambayo ni vielelezo vya namna anavyoisaliti jamii hii ni, kuvunjilia

mbali vyama vya wafanyikazi na vilevile kuvunjilia mbali mahakama za mahakimu. Taifa zima kwa jumla, limesawiriwa kuwa taifa lenye matatizo mengi; ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Matatizo ambayo yametokana na uongozi wa Kigogo. Ni dhahiri kwamba, usaliti huu unatokana na nguvu na uwezo wa viongozi.

Usaliti mwingine unajitokeza miongoni mwa wale wafungwa tisa waliokubali kuwa walishiriki katika uhaini. Kwanza, usaliti unaonekana miongoni mwao. Pwacha anamsaliti Haramia kwa kumweleza Dude mipango yao ya mle chumbani mwao. Haramia anawashawishi wakatae kuhusika katika uhaini na vilevile anawaeleza kwamba, wakubwa kama vile Kanali Bunju pia wamo. Huu ndio ujumbe Pwacha anaompelekea Dude, usaliti ambao unasababisha Haramia kuteswa kwa kuwekwa chumba kimoja na joka kule Mashakani Hotel ili joka lile limmeze angali hai.

Wafungwa hawa tisa pia wanasalitiwa na Kanali Bunju na wenzake. Akina Bunju waliwaahidi hawa wafungwa kwamba, wangewaachilia huru iwapo wangekiri kuhusika katika mauaji ya Kigogo. Mambo yanakwenda kinyume kwa sababu ahadi hiyo inakiukwa, hawa wanakuwa miongoni mwa washukiwa wanaohukumiwa kifo.

Kanali Bunju na wakubwa wengine serikalini wanawasaliti watu waliowatumia kuduhushi mambo na kuwapelekea habari. Haramia anasalitiwa na Bunju, mwandani wake wa siku nyingi, kwa kumshika na kumtuhumu kwa uhaini. Tunasoma:

> *Lakini siku Haramia aliyokamatwa, Kanali Bunju alimgeuka, akamruka huko, hamjui ndewe wala sikio. Kule kujiweka karibu naye, badala ya kumuafu kukamponza, Haramia akaonekana kama aliyetumwa na Kubwalao kujiingiza katika kaumu ya Kanali Bunju ili ayajue mambo yake, azijue nyendo zake, jasusi mkubwa aliyejipenyeza katika mambo ya watu. Na ndiyo maana akawa miongoni mwa watu wa mwanzo kukamatwa siku ile aliyouliwa Kigogo*
> *(uk. 164).*

Hatima ya Faraji ambaye ameajiriwa na Kapera nayo ni kama ya Haramia.

Wananchi wa kawaida wamesalitiana wenyewe kwa wenyewe. Katika Kiwango hiki cha usaliti tunawarejelea wale vibaraka ambao wameajiriwa na wakuu fulani serikalini kusikia wayasemayo watu. Mifano ni Faraji na Haramia. Jamii anayoizungumzia mwandishi imekumbwa na matatizo mengi, yeyote anayethubutu kusema jambo kuhusu matatizo haya hukamatwa na kufungiwa gerezani. Hii ndiyo kazi ya akina Haramia na Faraji ni wananchi wa kawaida wanaokumbwa na matatizo, badala ya kuungana na wenzao katika kutetea maslahi yao, wanatetea maslahi ya wadhulumu.Tunasoma: *"Kapera akamwajiri Faraji kwa posho ya shilingi mia mbili kwa mwezi. Kazi yake ni kumtafutia habari. Nani anasema nini, huyu anafanya nini, yule anaongea nini"* (uk 107). Haramia na Faraji ni mifano tu ya vibaraka wanaowasaliti wenzao kwa manufaa ya wenye mamlaka. Usaliti kama huu unaisaliti jamii yote na una misingi yake katika ubinafsi, kwani wanaoyatenda haya wanataka wanufaike kwa kuwa karibu na wenye mamlaka.

Kama tulivyosema, usaliti ni zao la ubinafsi. Ubinafsi ni hali ya kutowajali wengine kwa kujipenda wewe mwenyewe. Watawala na wenye mamlaka huwa tayari kufanya kila aina ya uhalifu na matendo ya kikatili ili kutimiza ndoto zao. Katika riwaya ya *Haini,* Kanali Bunju na Wakili Chopra ni mifano bora ya wahusika wanoendeleza ubinafsi. Tunamwona

Bunju akiongoza msako wa mahaini na kuendeleza dhuluma za hali ya juu dhidi yao akiwa na lengo la kujinufaisha mwenyewe. Anafanya haya yote kwa sababu ana lengo la kukikalia kiti alichokiacha Kigogo ingawa alikikosa. Tunasoma kuwa,, Bunju:

> *Alikuwa amekaa ofisini, peke yake, juu ya kile kiti chake. Anawaza, ilikuwaje Kigogo ameuawa na hakuna mwingine aliyestahili kurithi Kiti chake isipokuwa yeye, leo kiti hicho anakikalia mtu mwingine, siye yeye "vipi" ilikuaje? Yeye, mbabe wa kisiasa, shujaa aliyeongoza msako wa kuwasaka wauaji, akawatokomeza mmoja mmoja mpaka akawamaliza wote. Leo kiti cha enzi kimemtoka, anakikalia mtu mwingine....*
> *(uk 161 )*

Naye Chopra, mwendesha mashtaka wa serikali, ni barakala aliyetia fora ili kuyamudu maslahi yake mwenyewe. Tunaelezwa kwamba, kwa sababu ya ubarakala na hila zake aliaminiwa na mahasimu wote watatu waliokitawala kisiwa cha Zanzibar. Serikali ya Elizabeth wa pili ilimwamini kwa sababu ya utiifu wake kwa watawala uliokuwa wa kupigiwa mifano; Sultani na wafuasi wake nao walikuwa na imani kubwa na Chopra, na wakamfanya mshauri mkuu wa mambo ya kisheria; naye Kigogo akamfanya Chopra mwanasheria mkuu wa serikali yake. Namna ambavyo Chopra anawasaliti mahaini kwa kuendesha mashtaka ya uongo dhidi yao, kunamsawiri kuwa kielelezo cha viongozi ambao kwa kujali maslahi yao binafsi, wanawadhulumu kwa kutowajali watawaliwa. Hili ni dhihirisho la namna nguvu rasmi walinazonazo viongozi, zinavyotumiwa katika kuwakandamiza raia.

Kiwango kingine cha ubinafsi unaotokana na usaliti kinaonekana mle gerezani ambapo tunawaona Pwacha na wenzake wanane, wanakubali kuwasaliti akina Hamza ili kuokoa roho zao. Wanafahamu kabisa kwamba Hamza na wenzake hawana hatia kamwe, lakini wanaamua kuwaingiza katika shutuma za uhaini. Mbali na kuwa wamelazimishwa kufanya hivi kwa kudhulumiwa, pana ubinafsi kwa kuwa wamedhamiria kuokoa roho zao huku wengine wakiangamia, ingawa mambo yalitendeka kinyume na matarajio yao.

Jamii ya Kigereza ni jamii ambamo nguvu hutawala kwa kuidhibiti jamii. Kwa hivyo, suala la **nguvu rasmi** tulilotaja mbeleni, ni moja ya masuala makuu katika jamii ya aina hii. Usaliti unakuwa moja ya athari za jamii ya aina hii kwa kuwa viongozi wanatumia mbinu zote zilizoko ili kujihifadhi uongozini. Ndiyo sababu ya kuwasaliti wananchi wenzao kwa kuzisaliti sheria za nchi yao kunakuwa muhimu kwao ili kudumisha nafasi yao uongozini. Usaliti ainaaina unaojitokeza una misingi yake katika ubinafsi.

## 4.2 Hofu

Kamusi ya Kiswahili Sanifu ya TUKI (2004 ) inaeleza kuwa, hofu ni jambo linaloleta woga au kitisho. Mifumo ya kigereza ya kuadhibu iliyokita mizizi katika jamii za kigereza, ni mambo yanayozua hofu miongoni mwa wananchi wa tabaka la chini. Katika *Haini,* Shafi ameonyesha namna raia wanashikwa na kutiwa ndani wakati wowote, wawe na hatia au la. Jambo hili linawatia hofu. Uongozi unaosawiriwa katika *Haini* ni uongozi wa kiimla ambao umewatia wananchi hofu kwa kuwa ni lazima kila mwananchi aseme na kutenda kulingana na matakwa ya viongozi. Hofu imetawala kote; kwa walio gerezani na kwa walio nje. Mle gerezani mahaini wanakandamizwa sana kiasi kwamba, wanaishi maisha ya

hofu na kukata tamaa. Kule nje, maisha ya familia nyingi ni maisha ya Kigereza nje ya gereza, hofu imetawala kote, watu wote wamekuwa kama walio gerezani.

Mwandishi amesawiri matatizo yanayoikumba jamii hii, lakini kwa sababu ya hofu ya gereza, wananchi wamekaa kimya huku wanaumia nyonyoni. Kuna ukosefu wa bidhaa muhimu kama vile, mafuta, unga, sukari na kadhalika. Hakuna anayethubutu kuuliza kwa kuwa akisikika, atashikwa na kutiwa gerezani. Wananchi wanabaki katika hali ya hofu. Mwandishi ametumia maisha ya familia ya Khadija mkewe Hamza, kuonyesha namna hofu inavyolikumba taifa zima. Kwa mfano, Bi Farashuu anamwonya Khadija asiongee kwa sauti ya juu kuhusu matatizo ya kuvipata bidhaa kwa kuwa akisikika, atazua balaa. *"Usipige kelele wakakusikia likaja kutuzukia balaa jingine"* (uk. 147).

Usemi wa Abdul akiwa gerezani ni dhihirisho la namna utawala wa ukandamizaji katika jamii hii ulivyowatia watu hofu.

> *...katika nchi hii kila mtu ana wasiwasi, hujui saa ngapi utakamatwa ukatiwe ndani. Sukari hakuna, ukisema unatiwa ndani. Mchele hakuna, ukisema unatiwa ndani! Sasa maisha gani haya*
> *(uk 89)*

Tangu mwanzoni tunawaona watu wakishikwa ovyo ovyo kwa tuhuma za mauaji ya Kigogo. Wanapelekwa katika kituo cha polisi ambako wanapigwa na kuteswa kinyama. Mwandishi analisawiri kundi hili kuwa kundi linaloishi kwa hofu kuu na lililokata tamaa. *"Hakuna aliyezungumza na mwenzake kila mmoja akihofia maisha yake, kwani hakuna*

*hata mmoja aliyeweza kutabiri hatima yake katika hali ya kutisha kama ile...hakuna aliyekuwa na matumaini."* (uk 09).

Mhusika Haramia ambaye anaamini kuwa hawezi kusema uongo, anakiri mashtaka ya kushiriki katika uhaini na kuwa shahidi wa akina Kanali Bunju. Kukiri huku kwa Haramia na wenzake, kunatokana na hofu inayosababishwa na vitisho vikuu. Kwa mfano, kabla ya kupelekwa mahakamani wanatishwa kupigwa kila mmoja risasi na kuzikwa papo hapo.

> *Kanali Bunju na Kifupinyundo walipomaliza mazungumzo yao, Kanali Bunju akatoa amri, "Haya waleteni kila mmoja mbele ya kaburi lake". Walijipanga kila mmoja wakawaongoza kama wanaocheza gwaride wanaelekea kule yalipo makaburi. Nyuso wameziinamisha chini kama wenye kuwaonea haya mauti yanayowakabili, jasho linawatoka, nyoyo zao zinapiga mapigo ya mshtuko mkubwa, miguu inawatetemeka, manyoya ya mwili yamewasimama. Kanali Bunju alinyanyua sauti yake juu akawauliza kwa kelele, "Nakuulizeni mara ya mwisho! Mtakubali mtakataa!" "Tunakubali!" wote walijibu kwa umoja wao.*
> (uk 208 – 209).

Vitisho hivi vinawatia hofu na wanapofikishwa mahakamani, kila mmoja anakubali.

Hofu pia inadhihirika miongoni mwa wananchi pale baadhi ya watuhumiwa wanapofunguliwa. Mwandishi anaeleza kuwa, wanasherehekea kwa minong'ono wasije kuambiwa wanasherehekea kifo cha Kigogo. *"Kila mmoja alielekea kwake. Huko wakapokelewa kwa yo-yo yo, shangwe na vigelegele vya chini kwa chini wasijie wakaambiwa wanasherehekea wakati watu wamo maombolezo ya kifo cha Kigogo"* (uk 104). Hivi ndivyo Subet alivyokamatwa akituhumiwa kuwa anasherehekea kifo cha Kigogo kwa sababu alimchinja jogoo wake.

Hofu na vitisho ni sifa kuu zinazodhihirika katika jamii za Kigereza. Hii inatokana na sababu kwamba, jamii za Kigereza ni jamii ambamo watawaliwa wamedhibitiwa kwa nguvu rasmi zilizo mikononi mwa viongozi. Pamoja na hayo, mfumo wa Kigereza wa kuadhibu unaotawala katika jamii hizi ni mfumo wa kuhofisha. Hili ni jambo linalodhihirika katika maandishi mengi ya kifasihi na yasiyo ya kifasihi ambayo yamesawiri picha za mifumo ya aina hii ya utawala. Kwa mfano katika riwaya ya *Shamba La Wanyama* (1967), Orwell ameonyesha namna Mkimwa anavyotumia jeshi lake la mbwa kuwaangamiza wanyama waliokisiwa kuwa na uhusiano na Mzushi. Jambo hili linawatia wanyama hofu na kuwaacha wakiishi kwa hofu kuu. Maandishi mengi yanayozungumzia harakati za ukombozi barani Afrika kama vile ya Mandela. (1990), Sithole (1976), Hussein (1969), na mengine mengi yanaonyesha namna hofu na vitisho zilivyo sifa kuu katika jamii zilizodhibitiwa na tawala kandamizi.

Mfano mwingine wa jamii iliyokumbwa na hofu ni jamii anayoisawiri Mohamed katika tamthilia ya *Kivuli Kinaishi* (1990). Hii ni jamii inayotawaliwa na chama kimoja na kuendeshwa kwa dhuluma, mauaji na ukandamizaji. Watu wamenyimwa uhuru wa kusema hivi kwamba, hawaruhusiwi kujadili na kutoa maoni yao hadharani kwa sababu wanachelea kusikika wakiwa na maoni toafuti na yale ya Bi. Kirembwe. Hali hii ya kuchelea kusema hadharani ndiyo inayosababisha Bi. Kizee kuitoa hadithi kimya kimya kwa kuwa anawaeleza viongozi kuwa ni wenye uwezo, pato, hasira kali, wanaotisha na wenye kukosa imani au huruma.

Jamii anayoisawiri Shafi katika *Haini* ni jamii inayokumbwa na hofu, kutoka gerezani hadi katika jamii pana. Hofu hii inasababishwa na nguvu rasmi walizonazo watawala, ambao wanafanya kila jitihada kuwadhibiti watawaliwa kwa ajili ya maslahi yao wenyewe. Kwa kuwa hofu imetanda kote, watu wamepoteza imani yao kwa wenzao. Hakuna anyemwamini mwenzake kwa hofu kwamba, huenda akawa ni msaliti wake.

## 4.3 Ukosefu wa Haki

Jamii ya Kigereza anayoisawiri Shafi katika *Haini,* ni jamii ambamo mkondo wa haki umesalitiwa kwa matumizi mabaya ya nguvu na mamlaka ya watawala. Jambo hili linadhihirika gerezani na nje ya gereza. Gerezani namna washukiwa wa uhalifu wanavyodhulumiwa bila kupewa nafasi ya kujitetea kunadhihirisha ukosefu wa haki.

Msako wa mahaini unapotekelezwa, wanafungiwa na kuteswa kwa kosa ambalo wengi wao hawakuhusika. Wanateswa kwa siku nyingi kabla ya kufikishwa mahakamani. Kwa mfano, Hamza na wenzake ambao wameachiliwa huru kwa kutohusika, wameumia gerezani kwa jumla ya miaka miwili. Ni kweli kwamba, hawakutendewa haki kwa kudhulumiwa kwa sababu ya kosa ambalo halikuwahusu wala hawakujifahamu.

Shafi amesawiri picha halisi ya jinsi utawala wa jamii anayoindikia ulivyo. Ni jamii ambamo vyombo vya dola vinatumiwa kuwakandamiza wananchi. Hakuna sheria kwa wanyonge, chambilecho Foucault kuwa, sheria hutungwa kulinda maslahi ya viongozi walio wachache.

Idara ya magereza, mahakama na polisi ni vyombo vinavyotumiwa kuwakandamiza wananchi badala ya kuwalinda na kulinda haki zao. Asasi ya gereza inafaa kutumika katika kurekebisha tabia za wahalifu, huku mahakama nazo zikiwa na jukumu la kutekeleza haki. Polisi nao wanastahili kuwalinda wananchi. Katika jamii anayoisawiri Shafi, gereza ni mahali pa mateso, dhiki na hata maafa. Mahakama na polisi ni vyombo vinavyotumiwa na wenye nguvu walio wachache, kuwanyima wanyonge haki zao. Kwa mfano, tunaona namna Chopra, mwendesha mashtaka mkuu wa serikali anavyoendesha kesi ya uhaini dhidi ya washukiwa kwa hila kuu.

Hata hivyo, jambo la kufurahisha ni kwamba, haki inatekelezwa wakati wa hukumu ya kesi ya washukiwa wa uhaini. Kwanza, washukiwa wanapewa haki ya kusimama mbele ya mahakimu na kujitetea kadri ya uwezo wao. Vilevile, haki inatekelezwa kwa kuwafunguliwa kutoka gerezani wale washukiwa ambao hawakuhusika, kulingana na uchunguzi wa mahakama. Hamza, akiwa mmoja wa wanaofunguliwa, mwandishi anaonyesha namna haki inavyotekelezwa anapofunguliwa. Tunasoma:

> *Kutajwa kwa jina la Hamza kukafuatiwa na maelezo kutoka kwa Musadiq: "Hakuna asiyejua juu ya usuhuba wako mkubwa na Hamduni na hakuna atakayeamini kwamba, jinsi mlivyo wewe na Hamduni, Hamduni awe ndiye mwuaji na wewe uwe humo ...Hata mimi siamini kabisa kwamba wewe Hamza humo. Lakini uchunguzi umeonyesha hivyo na kwa hivyo mahakama inakuachia"*
> (uk 264)

## 4.4. Unafiki

Unafiki ni hali ya kujifanya kuwa ni rafiki hali ni adui, hali ya kutokuwa mkweli. Jamii anayoisawiri shafi katika *Haini* ni jamii iliyojaa unafiki mwingi. Kwanza, unafiki unadhihirika kupitia kwa mhusika Kanali Bunju. Bunju alikuwa rafiki mkubwa na Kigogo, lakini kulingana na Haramia, amehusika na mauaji ya Kigogo. Haramia anasema kuwa silaha ziliibwa kutoka kwenye ghala la kuzitunzia wiki nzima kabla ya mauaji, wakubwa wakajua hilo na hakuna lolote walilolifanya. Zaidi tunasoma kuwa, siku ya mauaji ya Kigogo Haramia alikuwa na Bunju lakini hakuonyesha wasiwasi hata kidogo.

Tunaelezwa kuwa Bunju alikuwa na usuhuba na marehemu Kigogo; Kigogo hakuenda popote bila kuandamana naye, hakufanya lolote bila ya kushauriana naye, Kigogo alikuwa hali akashiba kama hakumwona, hakupata usingizi kama hakukaa naye hadi usiku wa manane. Bunju alikuwa mwandani wake, msiri wake, aliyemkinai kwa mambo yake yote, ya siri na ya dhahiri. Huyu ndiye kiongozi ambaye hakuchukua hatua wakati silaha zilipoibwa wala kuonyesha wasiwasi siku ya mauaji ya Kigogo. Urafiki wa Bunju kwa Kigogo, umejaa unafiki kwa kuwa lengo lake lilikuwa kukikalia kiti cha Kigogo.

Kwa unafiki, akina Kanali Bunju wanawadanganya baadhi ya washukiwa kukiri kushiriki katika mauaji ya Kigogo kwa ahadi kwamba, wataponya roho zao huku akina Bunju wakiwa na lengo la kuwanasa na kuwaangamiza. Katika ofisi ya Kanali Bunju tunamwona Kanali Mapepe akimpembeleza Hamza akiri. Anasema:

*Sisi tunajua kwamba wewe huhusiki lakini ombi letu ni kutaka ukubali. Ujidai kama vile umo na unawajua wengine. Tuna orodha ya majina hapa tutakupa, na wote hao tumeshawatungia hadithi kuthibitisha jinsi wanahusika (uk. 82)*

Katika mazungumzo haya Hamza anaambiwa kuwa atakuwa shahidi tu kule mahakamani kisha aachiliwe. Huu ndio mtego uliowapata Haramia na wenzake wanane ambao badala ya kuachiliwa kama walivyoahidiwa wanahukumiwa kifo.

Unafiki mwingine unajitokeza kupitia kwa Kapteni Baraka. Baraka ni sahibu mkubwa wa Hamza. Amemuahidi Khadija kumpa habari za Hamza lakini Khadija anapoenda kwake, anamfanyia unafiki. Baraka na mkewe wanamdanganya Khadija kuwa, Baraka amesafiri na hatarajiwi kurudi hivi karibuni. Huu ni unafiki kwa kuwa ukweli ni kwamba Baraka yumo, shida ni kwamba hataki kuhusishwa na Hamza aliyetuhumiwa uhaini.

Azizi naye anamfanyia Khadija unafiki. Anatumia nafasi ya hali ngumu iliyomkabili Khadija kutaka kumdhulumu kimapenzi. Huku Khadija akiwa na imani kwamba, huenda Azizi akamfaa katika kumkomboa Hamza, Azizi ana nia tofauti. Mganga, Kidongo Chekundu naye anamfanyia Khadija unafiki kwa kumhadaa kwamba, atamfanyia dawa ya kumkomboa Hamza.

Katika jamii za kigereza, unafiki ni moja ya mbinu inayotumiwa hasa na watawala katika kuwakandamiza watawaliwa. Viongozi wengi katika jamii za aina hii hutumia hila na ujanja katika kutawala ili waweze kuwadhibiti watu. Tumeona namna watu

wanavyotuhumiwa uhalifu ili viongozi wawe na ushahidi wa kuwakamata na kuwafungia. Ukweli ni kuwa, tuhuma hizi zinaelekezwa kwa kundi fulani la wanajamii ili waweze kutengwa na wengine.

Unafiki unajitokeza kama zao la nguvu kwa kuwa unatekelezwa na watu walio na uwezo au mamlaka ya namna fulani. Kanali Bunju na wenzake, Kapteni Baraka na Azizi ni mifano ya wahusika wanaotumia mamlaka yao kuwafanyia wengine unafiki. Usaliti unaojitokeza katika jamii hii ni zao la unafiki. Kadri mifumo ya jamii inavyoendelea kufanya kazi kigereza, unafiki utaendelea kuwepo, chambilecho Shafi, *"Mnafiki hawachi unafiki kwani unafiki ni ila isiyosarifika".*

(uk. 205)

## 4.5 Jitihada za Ukombozi

Foucault aliamini kuwa, lengo kuu la kuishi ni mtu kuwa huru. Aliamini kwamba, kutimiza lengo hili ni lazima kila mara mtu apambane na adhabu za kijamii. Jamii anayoiandikia Shafi imesawiriwa kuwa jamii ambayo imekumbwa na mapinduzi ya serikali mara kwa mara. Utawala wa Elizabeth wa pili uliondolewa mamlakani na Sultani. Naye Sultani na wafuasi wake, walitimuliwa na wakulima na wakwezi ambao walimpa Kigogo uongozi wa nchi yake. Leo kumekuwa na jaribio la kuiangusha serikali ya Kigogo ambalo limesababisha kifo cha Kigogo. Michafuko hii inayosababisha mapinduzi ya serikali ya mara kwa mara, inasukumwa na dhamiri ya raia kutaka kujikomboa kutoka kwa utawala dhalilishi.

Katika jamii ambazo mifumo ya Kigereza imekita mizizi, mna mateso mengi kwa wanajamii kiasi kwamba, inawatia wanyonge msukumo wa kujikomboa. Sururu anajaribu kutoroka gerezani kwa sababu ya jitihada za kujikomboa.

Mwandishi akiwa anazungumzia matatizo mengi ya kisiasa na kiuchumi yanayoikabili jamii hii, mauaji ya Kigogo kwa wengine yanaonekana kama njia moja ya kujikomboa. Mle gerezani Abdul anasema, *"Bora walivyomtoa roho. Heri upatikana ndani ya tumbo la shari. Sisi ni muhanga! Muhanga ili wengine wapate nusura"* (uk.89)

Katika jamii za Kigereza, jitihada za ukombozi mara nyingi hugonga mwamba na wanaoongoza jitihada hizo, huishia kufungiwa gerezani kama njia ya kuwaadhibu na kuwatenga wasiwaathiri wengine. Kutofaulu kwa jitihada hizi hutokana na sababu kwamba, jamii za Kigereza ni jamii zilizodhibitiwa hofu na vitisho hutawala na watawala wana vyombo vya kuchunguza mienendo ya watu. Kazi nyingi za fasihi ya gerezani ambazo tumezisoma, Mathalan kazi za, Sithole ( 1976), Kihoro ( 1998), Kinyatti. (1996), Mandela ( 1990) na Jackson (1971) na Thiong'o. (1981) zinaonyesha kuwa waandishi hawa ni mifano ya baadhi ya wanyonge waliiongoza jitihada za ukombozi lakini wakaishia kufungiwa gerezani, kwa kuwa jamii zao ni jamii zilizodhibitiwa na mifumo ya Kigereza.

## 4.6 Hitimisho

Jamii ya kigereza ni jamii ambamo mifumo yake hufanya kazi Kigereza. Ni jamii ambamo, sifa zake kuu kama anavyozijadili Foucault katika *Discipline and Punish* (1977), za **nguvu, kuadhibu na uchungulizi,** ndizo kaida kuu za maisha ya kila siku. Ni jamii

ambamo viongozi hutumia kaida hizi katika kuyadhibiti maisha ya watu kwa maslahi yao binafsi.

Kwa mujibu wa *Haini,* mifumo ya jamii inapofanya kazi Kigereza, kama tulivyoona, hujenga jamii iliyojaa usaliti, ubinafsi, kutoaminiana, watu kuishi kwa hofu, unafiki na jitihada za watu za kujikomboa hugonga mwamba kwani jamii hii huwa imedhibitiwa kabisa. Hali hii huzua matatizo mengi kwa wanajamii; kisiasa, kiuchumi, kijamii na kisaikolojia.

Kisiasa, uongozi katika jamii hii ni wa kiimla na kandamizi. Viongozi wanatumia mamlaka yao katika kuwakandamiza wananchi ili kuwadhibiti. Kiuchumi, jamii hii ya Kigereza kama ilivyo katika *Haini,* ni jamii iliyotumbukia katika janga la umaskini, jamii ambamo bidhaa za kimsingi kama vile unga, sukari na mchele havipatikani kwa urahisi. Ni jamii ambayo imekumbwa na matatizo mengi ya kijamii. Mfumo wa gereza wa kuadhibu umewatenga wafungwa na familia zao. Mbali na kuunda usugu miongoni mwa wahalifu, familia zimesambaratika kwa kuwa waume na wake wao wametenganishwa. Hali hii imesababisha matatizo mengi ya kisaikolojia kwa watu walio gerezani na walio nje. Walio gerezani na walio nje wanaumia ndani kwa ndani.

Kwa jumla, jamii ya kigereza kama inavyosawiriwa katika *Haini* ni jamii ambamo raia walio wengi wamedhibitiwa na viongozi wao kwa kuwa wana nguvu rasmi. Raia hawa wamekata tamaa na wanaishi katika maisha ya hofu kuu. Kwa maoni yetu, athari za jamii

ya kigereza ambazo tumezichunguza katika sura hii, ndizo zinazojitokeza katika *Haini* na zingine zote zinaweza kufungamanishwa nazo au zimetokana na, na kusababishwa nazo.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Hitimisho

Tasnifu hii, imechunguza namna taswira ya gereza inavyotumiwa kuendeleza maudhui katika *Haini*. Tumeeleza maana ya taswira na mbinu nyingine za kifasihi ambazo zinaafikiana kimaana na mbinu hii. Katika utafiti huu, tumetumia sitiari kama kisawe cha taswira ambayo pia huitwa jazanda kwa mujibu wa baadhi ya wataalamu na wahakiki wa fasihi. Vilevile, tumefafanua dhana ya gereza pamoja na dhana ya jamii ya Kigereza. Ufafanuzi wa dhana hizi umekuwa muhimu kwa kuwa umetuwekea msingi na mwelekeo wa kuchunguza maudhui ya jamii ya Kigereza katika *Haini.*

Kwa mujibu wa utafiti wetu, tumegundua kwamba pana mwingiliano wa kiwango kikubwa baina ya gereza na jamii pana. *Haini* imetuwezesha kumulika wazo hili kwa kuwa usimulizi wake umejengwa katika mazingira ya kigereza ambayo yametuwezesha kufananisha maisha ya gerezani na maisha yaliyo nje ya gereza. Hii ndiyo sababu tumetumia gereza Kistiari ili ituwezeshe kuangazia pande hizo mbili.

Jamii ambayo Shafi ameisawiri katika *Haini*, ni jamii ya Kigereza. Shafi ametumia tukio la kufungwa kwa Hamza na wenzake kwa shutuma za uhaini kama msingi wa kuiangazia jamii hii. Ameliangazia gereza la Kinoamiguu, walimofungiwa washukiwa. Gereza hili, anavyolisawiri Shafi ni lindi la mateso. Limegawanywa katika vitengo mbalimbali vya

matesc.Mathalani; washukiwa kufungiwa ndani ya vyumba vyenye mazingira dhalilishi; Mashakani Hotel; Chumba cha kiza; na vipigo vya kwa Ba Mkwe.

Jamii inayotuhumiwa uhaini imesawiriwa kuwa jamii dhaifu isiyo na mtetezi. Maisha yao, yamo mikononi mwa askari jela na wanajeshi. Imesawiriwa kama jamii iliyobobeshwa katika upeo wa ukatili. Kupigwa kwa fimbo za mipera, kutiwa hofu, kinyimwa chakula bora na hata kuuawa ndizo dhuluma zinazoendelezwa dhidi ya jamii hii. Ni jamii ambayo imekolezwa mateso ya kisaikolojia.

Kwa kiasi fulani, Shafi ameyatoa masimulizi yake nje ya gereza na kutuonyesha namna maisha ya jamii pana yalivyo. Kule nje, raia wa kawaida wanaishi kwa hofu na mateso: Ni wanyonge wa kila hali, wamejaa huzuni; wamekumbwa na njaa, kukamatwa wakati wowote na vilevile kukolezwa mateso ya kisaikolojia. Jamii iliyo nje ya gereza imesawiriwa kama iliyomo katika gereza moja pana. Hali hii imesababisha hofu, umaskini, kusambaratika kwa familia, usaliti, unafiki, ubarakala na kutoaminiana miongoni mwa raia hawa.

Uchunguzi wetu umeongozwa na nadharia ya Ki-Foucault, ambayo kama tulivyotaja mwanzoni, mihimili yake mikuuu ni masuala ya **nguvu, gereza, adhabu, uchungulizi na udhibiti**. Shafi ametuwezesha kuelewa namna masuala haya yanavyojitokeza katika jamii zetu. Riwaya hii, imeonyesha kile ambacho Foucault amekitambua kama kubadilika kwa adhabu kutoka kwa ile ya kimwili hadi kwa ile ya kiakili; yaani adhabu sio mateso tu, bali

pia ni njia pana ya kudhibiti. Hali hii inadhihirika katika *Haini* kwa namna ambavyo umma ulivyodhibitiwa kutokana na hofu inayolikumba taifa.

Riwaya hii imesawiri gereza kama jukwaa la kuonyesha namna nguvu rasmi zinavyojidhihirisha katika jamii za kisasa. Maelezo ya mwandishi kuhusu dhuluma wanazofanyiwa washukiwa mle gerezani, yanatuwezesha kuelewa namna nguvu hizi zinavyofanya kazi katika jamii ya Kigereza. Kuadhibu, kama njia ya kudhihirisha nguvu hizi, imechukua nafasi kuu katika usimulizi wa Shafi. Katika kilele cha kuwasaka washukiwa, adhabu imekuwa njia ya kudhihirisha nguvu za watawala. Kwa mfano, Kanali Bunju anadhihirisha uwezo mkubwa wa nguvu alizonazo kwa kumwaga damu ya raia wengi bila huruma wala majuto.

Uchunguzi huu umebainisha namna serikali ilivyoweka mikakati mbalimbali ya kuwadhibiti watu, hasa kwa kuchungulia na kuchunguza mienendo yao. Serikali inatumia mbinu ya ujasusi katika kufanikisha jambo hili. Raia wanaokaidi matakwa ya utawala, wanaadhibiwa kwa kifungo na mateso. Mbinu hii ya kuwachungulia raia na kuwadhibiti, ni sitiari ya mnara wa ulinzi, unaotekeleza jukumu la kuwadhibiti wafungwa gerezani kulingana na nadharia ya Ki Foucault.

Aidha, uchunguzi wetu umebainisha kuwa, mawazo ambayo Shafi anayazua katika kazi yake yametokana na tajriba zake kuhusu jamii ya Zanzibar – kihistoria,kijamii na kisiasa. Katika kazi hii, amegusia masuala ya mahusiano ya nguvu katika jamii hii, tangu enzi ya utawala wa Malkia Elizabeth, utawala wa Sultani na utawala wa baada ya mapinduzi. Kiini cha riwaya hii ni tukio la kihistoria la kuuawa kwa Rais Abeid Karume wa Zanzibar mnamo 1972.

Tunapoitathmini *Haini,* hatuna budi kusema kwamba, mawazo ya nadharia ya Ki-Foucault yanaafikiana na hali ilivyo katika jamii anayoizungumzia Shafi. Vilevile, hatuna budi kuhitimisha kwa kusema kwamba, mwandishi ameonyesha mfanano uliopo baina ya gereza na maisha yaliyo nje ya gereza. Kwa hivyo, gereza ni sitiari ya jamii pana.

Hadi kiwango hiki, ni dhahiri kwamba nadharia tete na madhumuni ya uchunguzi wetu yameafikiwa.

## 5.1 Mapendekezo

Uchunguzi huu umeshughulikia maudhui ya jamii ya Kigereza kwa kiwango na namna ambayo kwa maoni yetu, inaridhisha. Hata hivyo, hatuwezi kusema tumelishughulikia suala hili kwa ukamilifu wala hakuna yeyote anayeweza kudai kwamba, amefanya uchambuzi uliokamilika wa kazi fulani ya kifasihi. Katika fasihi, kuna mambo mengi ya kuchunguzwa katika kazi yeyote ile. Katika misingi hii, yapo mambo mengine mengi ya kufanyiwa uchunguzi kuhusu maudhui katika riwaya ya *Haini.* Vilevile, *Haini* inafaa ichunguzwe kwa upande wa fani ili kuonyesha namna mbinu za kisanaa zinavyotumiwa kukuza na kuendeleza maudhui katika kazi hii.

Utafiti huu ni muhimu katika fasihi ya Kiswahili kwa jumla kwa kuwa, umetoa mchango katika pengo lililokuwepo la uhakiki wa suala la jamii ya kigereza katika misingi ya nadharia ya ki-Foucault. Huu ni mchango muhimu kwa kuwa suala hili na nadharia hii ni mambo yatakayofaa tafiti za baadaye katika nyanja hii.

## Marejeleo


Abdalla, A. (1973) *Sauti ya Dhiki*. Nairobi: OUP.

Abramowitz, I. (ed) (1946) *The Great Prisoners. New York: E.P. Dutton & company, INC.*

Alper, B. (1974). *Prisons Inside Out.* Cambridge Bellinger Publishing Co.

Beiderwell, B. (1992) *Power and Punishment in Scott's Novels.* London: The Univeristy of Georgia Press.

Bentham, J. (1951) *A Fragment on Government.* London: Oxford University Press.

Buntman, F. (2003) *Robben Island: Prisoner Resitstance to Apartheid.* Cambridge: CUP.

Dreyfus, L. na Rabino, P. (1982) *Michel Foucault: Beyond Structuralism and Hermeneutics.* Hertfordshire: The Harvester Press Ltd.

Drolet, M. (ed) ( 2004) *The Postmodernism Reader* London: Routledge.

*Encyclopedia Americana* (Vol. 11) (1979) New York: Americana Corporation

*Encyclopedia Americana* (Vol. 22) (1979) New York: Americana Corporation

Encyclopedia *New Universal Library* (Vol. II)(1967) London: International Learning Systems Corporation Limited.

Foucault, M. (1972) *The Archeology of Knoweldge* London: Tavistock Publications Ltd.

____________ (1977) *Discipline and Punish: The Birth of the Prison*. London: Allen Lane.

Freire, P. (1972) *Pedagogy of the Oppressed*. Middlesex: Penguin Books.

Hazelrigg, L. (ed) (1968) *Prison Within Society*. New York: Anchor Books, Doubleday and Company Inc.

Hussein, E. (1969). *Kinjeketile*. Dar es Salaam. OUP.

____________ (1971). *Mashetani* Dar es Salaam: Oxford University Press.

Jackson, G. (1971). *The Prison Letters of George Jackson*.London: Ebenezer Bayles and Son Ltd.

Kamunde, M. (1983) "Kilio cha Wanyonge, Katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed": Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Kezilahabi, E (1990) *Nagona*. Dar es salaam: Dar es salaam Univeristy Press.

__________ (1991) *Mzingile*. Dar es salaam: Dar es salaam Univeristy Press. Publishers.

Kihoro, W. (1998) *Never Say Die: the Chronicle of a Political Prisoner*. Nairobi: East African Educational

Kinyatti, M. (1996) *Kenya: A Prison Notebook*. London: Vita Books.

Kitsao, J. (1982) "An Investigation of Themes in Swahili Literature: An Application of Stylostylistics in Chosen Literary Texts", PhD Thesis, UoN. (Haijachapishwa).

Mandela, N. (1990) *Nelson Mandela: The Struggle is My Life*. London: IDAF Publications Ltd.

Mazrui, A. (1988) *Chembe Cha Moyo*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mbatiah, M. (1999) "Development of the Swahili. Thesis Novel in Tanzania" Tasnifu ya Ph.D Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

__________ (2001) *Kamusi ya Fasihi.* Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Mirieri, E. (1993) "Kifo Katika Uendelezaji wa Maundhui Katika Riwaya za Kiswahili" Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Mkangi, K. (1984) *Mafuta.* Nairobi: East African Educational Publishers.

__________ (1995) *Walenisi.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Mohamed, S. (1990) *Kivuli Kinaishi.* Nairobi: OUP

Mosoti, M. (1993) "Maudhui Katika Riwaya nne za Emmanuel Mbogo". Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Mulokozi, M. (1997) "Miradi Bubu ya Wazalendo (Gabriel Ruhumbika)" Katika *Kiswahili Dar es Salaam: TUKI*

Nekesa, E. (2002) "Treatment of the theme of Childhood in Njabulo S. Ndebele's *Fools and Other Stories.*Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Njogu, K. (1997) *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar.*

Nairobi: Univeristy of Nairobi Press.

Nyaigoti, C. (1987) *Wingu Jeusi.* Nairobi: Heinemann.

Obiencha, E. (1975) *Culture, Tradition and Society in the West African Novel*. London: CUP.

Omuteche, J. (2004) "Mediated plot in the Construct of the theme of struggle in Nelson Mandela's autobiography, *Long Walk to Freedom.* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Oruka, H. (1976) *Punishment and Terrorism in Africa.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Orwell, G. (1967) *Shamba la Wanyama.* Nairobi: Kenya Litho Ltd.

Rice, P. na Waugh, P. (ed) (1989) *Modern Literary Theory.* London: Edward Arnold.

Sarara, M. (1997) "Maudhui katika Tamthili za S.A. Mohamed" Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Shafi, A. (1978) *Kasri ya Mwinyi Fuad* Dar es Salaam. Tanzania Publishing House.

___________ (1979) *Kuli.* Dares Salaam. Tanzania Publishing

House

____________ (2003) *Haini*. Nairobi. Longhorn Publishers.

Sithole, N. (1976) *Letters from Salibury Prison*. Nairobi: Trans-Africa Publishers.

Thiongo, N. (1981) *A Writer's Prison Diary*. Nairobi: Heinemann.

Trivedi, H. (1984) *The American Political Novel: Critical Essays*. New Delhi: Allied Publishers.

TUKI (2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi Oxford Univeristy Press.

Wafula, R. (1999) *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo Yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. (2002) *Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

____________ (2003) *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Focus Books.

Wellek, R. na Warren, A. (1949) *Theory of Literature:* Harcourt: Penguin Books.